Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Saba – Tarehe 21 Juni, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2012, Kitabu cha Kwanza *(Volume I).*

Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kwa

Mwaka wa Fedha 2010/2011, Kitabu cha Pili *(Volume II).*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo kwenye Kanuni yetu, Maswali kwa Waziri Mkuu, hamwulizi habari za vijijini kwenu wala habari za Majimboni kwenu au daraja la nyumbani kwenu, hahusiki na hayo. Mnauliza mambo ya Kisera, ambayo Waziri Mkuu kwa vyovyote vile anapaswa kuyafahamu. Kwa hiyo, naomba sana tusifike mahali nikakwambia hili swali unafikiri ni sahihi, wale wote walioomba hapa naomba mzingatie hivyo. Kama unataka kuuliza daraja la nyumbani kwako hapa siyo mahali pake, subiri wakati wa Sekta inayohusika.

Kwa kuwa leo tuna Kiongozi wa Upinzani kawaida yetu yeye ndiyo anaanza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali la kwanza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwa muda mrefu sasa yamekuwepo malumbano kati ya Madaktari na Serikali na malumbano kati ya Walimu na Serikali. Hivi tunavyozungumza sasa makundi haya mawili muhimu sana katika Utumishi wetu wa Umma yametangaza kufanya mgomo katika siku za karibuni. Tunaamini chini ya Uongozi wako na uratibu wako, Serikali ilishafanya mazungumzo na Walimu na imeshafanya mazungumzo na Madaktari. Tunajua katika hatua hiyo, mojawapo ya

dai la Madaktari la kumtaka Mganga Mkuu aondoke, Katibu Mkuu aondoke, Naibu Waziri aondoke na Waziri mwenyewe wote waliondoka wameingia wapya lakini tatizo lipo pale pale, kitu ambacho kinaweza kuashiria kama ni tatizo la mfumo kuliko tatizo la watendaji wenyewe.

Naomba kukuuliza ni nini hicho ambacho Serikali ilikubaliana kwa sababu mpaka leo haijatoa tamko rasmi ni nini ambacho ilikubaliana katika madai ya Madaktari na ni nini ambacho mlikubaliana katika madai ya Walimu? Je, ni yapi ambayo yameshatekelezwa na yapi hayajatekelezwa na ni kwa nini hayajatekelezwa na Serikali ina mpango gani wa kuyatekeleza? Nashukuru.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa maswali yote mawili.

Niseme kwa kifupi tu kwamba ni kweli tumekuwa na mgogoro wa Madaktari. Kama ambavyo taarifa za awali zilisema, tumekuwa tukizungumza nao kwa kipindi chote cha tatizo hili kwa lengo la kuona kama tungeweza tukafikia mwafaka. Kwa hiyo, kama mwezi mmoja hivi uliopita, ile Tume tuliyokuwa tumeiunda ambayo ilikuwa imejumuika na wao Madaktari ilimaliza ile kazi, baada ya kumaliza waliwasilisha taarifa yao Serikalini. Katika mambo kumi ambayo yalikuwa yameombwa na Madaktari, mambo kama matano hivi walielewana. Maeneo matano ndio yalikuwa bado yanaleta mvutano. Kwa hiyo, tulichofanya tukaiomba Wizara inayohusika, wajaribu kukutana nao kwa

maana kwamba, Timu ya Kitaalam imemaliza kazi yake, jukumu sasa ni juu ya Serikali yenyewe kuamua katika maeneo yaliyotofautiana hatua gani stahiki zichukuliwe.

Kwa hiyo, walifanya juhudi, Waziri alijitahidi kujaribu kuonana nao lakini haikuwezekana. Nikamshauri awaandikie barua tukaandika, bahati nzuri wakajibu lakini walichojibu kwa kifupi ni ile tu kwamba tumekuwa na mazungumzo na Serikali sasa kwa karibu miezi mitatu sisi hatuoni kama kuna haja ya kuendelea na mazungumzo.

Serikali iliona kwamba, pengine hapa tulipofika turejee kwenye utaratibu tuliokuwa tumekubaliana. Kwa hiyo, tuliomba turudi *CMA* ambao ndiyo chombo ambacho tulikuwa tumeanza nao mazungumzo ili baada ya kuwa inaonekana maeneo haya hatukukubaliana, basi turudi kule ili tuweze kupata utaratibu wa kisheria na tuweze kujenga hoja upande wa Serikali tuone tutaafikiana namna gani.

Kwa hiyo, kwa taarifa niliyonayo, wote walikwenda *CMA* makundi yote mawili na *CMA* imeamua kwamba jambo hili sasa litakwenda kwenye Mahakama ya Kazi. Kwa hiyo, tunasubiri maelekezo hayo kama nilivyoambiwa ni sahihi, basi sisi tutakwenda Mahakama ya Kazi na huko ndiyo tutakakolimaliza jambo hili.

Nataka niseme tu kwamba, yapo maeneo mengi ambayo wao walitofautiana, ambayo sisi Kiserikali tuliona bado yana nafasi ya kuweza kujadiliana nao.

Kwa bahati mbaya, hapakuwepo ushirikiano tulioutarajia katika ngazi ya Waziri; na niwakumbushe tu kwamba Waziri ndiyo ameingia pale safari hii kutokana na vurugu zilizokuwepo. Kwa hiyo, tulidhani ingesaidia sana kama wangemwona kwamba ni Kiongozi mpya wakashirikiana naye, waone ana mawazo gani juu ya tatizo hili. Bahati mbaya hilo halikujitokeza kwa kiasi hicho. Kwa hiyo, kwa upande wa madaktari tupo katika hatua hiyo na naamini tukienda huko, Serikali itatoa maoni yake juu ya maeneo fulani fulani ambayo naamini chombo kile kitatusikiliza.

Kwa upande wa Walimu, naweza nisiwe na maelezo mengi ya kusaidia sana, kwa sababu kilichotokea ni kwamba, yapo madai ambayo wangependa wakutane kama ilivyo utaratibu ili waweze kujadiliana kupitia chombo cha majadiliano. Kwa taarifa nilizonazo inaonekana chombo hicho baadhi ya Wajumbe wake walikuwa ama muda umefika kwa hiyo kilikuwa hakijatengenezwa; lakini juzi niliarifiwa na Katibu Mkuu Idara Kuu ya Utumishi kwamba, chombo kile sasa kipo tayari na wanaweza wakaenda kwenye majadiliano kulingana na utaratibu wa kisheria wa majadiliano. Kwa hiyo, hapo ndipo tulipo, ingawa nimeona sasa kuna *message* zinapita kwenye simu zetu ambazo mimi nasema pengine tusiharakishe kwenda huko, njia rahisi ni kufuata taratibu za kisheria na jambo litamalizika.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeliambia Bunge lako na Taifa kwamba kuna mambo matano mlikubaliana na mambo matano pengine bado hamjaafikiana. Kwa ajili ya ufahamu wa

Taifa; ungeweza kutuambia ni mambo gani ambayo mlikubaliana na ni yapi ambayo hamkukubaliana; na kwamba maadam mgomo wa Madaktari umepangwa kuanza Siku ya Jumamosi; huu mlolongo wa ki-*bureaucracy* wa kutupeleka mpaka Jumamosi unafikiri mpaka Jumamosi tatizo hili litakuwa limesuluhishwa tusirudishe tena Taifa kwenye mgogoro ambao upo?

**SPIKA:** Nadhani kuna timu inayo-*negotiate;* sasa sijui kama Waziri Mkuu unajua hilo *too specific*?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwamba, tatizo hili lilipofikia hatua fulani tulilazimika kwenda kwenye vyombo vya sheria, siyo kwamba tulikuwa tunazungumza bila kufuata utaratibu. Tuliamua turudi kwenye taratibu za kisheria, kwa hiyo, tukaenda kwenye chombo hiki ambao ni *CMA*, chombo cha majadiliano kile. Tulipokuwa katika hatua hiyo, baadaye Serikali yenyewe ikasema jamani kwa nini mnataka twende huko? Kwa nini tusikae tuzungumze tukubaliane? Ndiyo msingi wa kuunda ile Timu ya Pamoja. Tulitakiwa tukishakubaliana turudi *CMA* kwenda kusajili makubaliano ili yawe ndiyo makubaliana sasa kati ya Madaktari na Serikali.

Kama nilivyosema, baada ya taarifa ile kupatikana, Waziri kwa juhudi alizofanya imeshindikana. Imebidi turudi tena huko huko kwenda kutoa taarifa kwamba katika mambo kumi, matano yameonekana kwenda vizuri na haya matano mengine bado. Kwa hiyo, nadhani tulikofika dawa ni kwenda huko kwa taratibu za kisheria.

Sasa kama unazo taarifa hizo kwamba Jumamosi watagoma, watakuwa wanagoma, lakini ni kinyume cha utaratibu wa sheria. Mimi nadhani hilo ndiyo litakalojitokeza katika hatua hiyo. Nigewasihi sana, hakuna sababu ya kufika huko kwa sababu msingi wenyewe unaeleweka na ipo nafasi nzuri ya kuweza kuzungumza na kufikia mwafaka kama watakuwa na dhamira ya kweli.

Sasa unataka kujua ni maeneo gani, maeneo mengine uliyataja wewe mwenyewe; kulikuwa na *demand* kwamba uongozi pale wanaona kama vile hawajali na kwa hiyo ni vizuri wakajiondoa, *fine* wameondoka. Kulikuwa na maeneo mengine ambayo tulishakubaliana tangu mwanzo; kwa mfano, *on call allowance* tulikuwa tumeshaanza kuiendesha. Kulikuwa na suala la malipo kwa ajili ya *post-mortems,* nalo hilo lilionekana halina tatizo baada ya kupandishwa kutoka shilingi 50,000 kwa Wasaidizi na shilingi 100,000 kwa Madaktari Bingwa. Maeneo mengine siwezi kuyakumbuka kwa sababu ilikuwa ni *detailed*, lakini matano yanayobaki ni pamoja na mishahara, kuna posho zile ambazo walikuwa wanazihitaji za *transport, housing allowance, risk allowance* na *hardship allowance* na maeneo mengine kama hayo. Hayo ndiyo yalikuwa bado yamebaki kwa ajili ya majadiliano.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, naomba nikushukuru wewe binafsi. Pili, namshukuru Katibu wa Bunge, kwa msaada

mkubwa mlionipa wakati nikiwa naumwa mpaka leo hii nimerudi tena Bungeni. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwa muda mrefu Wafanyakazi wamedai mafao hapa nchini na hawajawahi kulipwa hata siku moja. Serikali itawalipa lini Wananchi ambao wanadai haki ambao wamefanya kazi kwenye mashirika mbalimbali na makampuni mbalimbali ambao hawajapata mafao yao?

**SPIKA:** Wafanyakazi wote kwa ujumla; haya.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Stephen Ngonyani, swali lake juu ya fidia. Kabla sijaenda huko, kwanza, nimpe pole maana Mwenyekiti wangu wa Kamati huyu, Kamati yetu mnaijua maarufu sana. Nilipokwenda kumwona Hospitalini nilimwambia vipi mwenzangu mambo yameshindikana kiasi hiki kweli maana wewe ndiyo mwenyewe tena, akaniambia leo sina ujanja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya tu swali ni la jumla sana, kwa hiyo, inawezekana na jibu lenyewe likawa la jumla tu. Kwa maana kwamba ni kweli katika baadhi ya maeneo yapo madai mbalimbali yanatokana na maswali mbalimbali yanayohusu watumishi. Kwa hiyo, ambacho tumekuwa tukifanya muda wote ni kuyapokea, tunayachambua, tukijiridhisha na yale madai yao, tumekuwa tunafanya hivyo hatua kwa hatu tunawalipa. Tumetokea kwa

Walimu. Upande mwingine Madaktari ambao tulikuwa na malimbikizo mbalimbali.

Kwa hiyo, inategemea ni kundi lipi na ni nini hasa unajaribu kukisema. Kwa ujumla, yapo matatizo ya namna hii lakini yanashughulikiwa kulingana na taratibu za Serikali.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, katika kundi moja la Mamlaka ya Mkonge Tanzania, kuna wafanyakazi wengi wamefanya kazi katika Mamlaka ya Mkonge, haki zao mpaka leo wanazitafuta na hawajui watazipata wapi. Je, Serikali inasema nini kwa hawa waliokuwa wanafanya kazi kwa muda mrefu ndani ya Mamlaka ya Mkonge? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina jibu la haraka haraka kwenye swali hilo. Ninachoweza kukuahidi ni kwamba, Mamlaka ya Mkonge kama unavyojua ilikufa siku nyingi na kwa hiyo, nadhani itakuwa ni jambo la miaka mingi kidogo. Acha tulitazame na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, tuone ni kundi lipi, nini wanatudai na namna tutakavyoweza kulishughulikia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 10 Mei, 2012 ulipofanya ziara Mkoani Mbeya ulipata Taarifa ya Mkoa na katika Taarifa hiyo moja ya jambo ambalo

ulielezwa ni tatizo linaloendelea kwa Mkoa Mzima wa Mbeya na maeneo mengine yanayolima Kahawa katika nchi hii. Tatizo lililopo Mbeya ni uuzaji wa kahawa mbivu (*red cherry)* na wewe katika kujibu uliagiza Mkuu wa Mkoa kwa sababu lipo tatizo kati ya wanaotaka kahawa hii inunuliwe na wale ambao wanataka isinunuliwe. Wewe ukaagiza kwamba waendelee kuzungumza ili tufikie mwafaka.

Siku chache baadaye kwa maana ya mwezi wa tano mwishoni, Bodi ya Kahawa ikatoa leseni ya kuruhusu ununuzi wa kahawa mbichi; je, agizo lako ulilotaka Serikali ya Mkoa iendelee kuzungumza ili kufikia mwafaka limepuuzwa? Unawaambia nini Wana-Mbeya na Watanzania kwa ujumla? (*Mkaofi*)

**SPIKA:** Nakuruhusu kwa sababu nasikia ulikuwepo huko.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Godfrey Zambi; lipo tatizo la Zao la Kahawa pale Mbeya. Tatizo lenyewe ni hili linalohusu uuzaji au ununuzi wa Kahawa mbichi. Kahawa Mbichi kwa maana kwamba, inakuwa haijaondolewa ganda lake, ukilinganisha na uuzaji wa kahawa ambayo imekobolewa na sababu yake kubwa ni kwamba, iliyokobolewa inaongeza thamani, jambo ambalo wote tunalijua. Ile ambayo haikukobolewa ni dhahiri kabisa kwamba bei yake inakuwa ndogo na kwa hiyo, mkulima ananyonywa, jambo ambalo muda wote tumekuwa tukilikataa.

Sasa nilijaribu kulifuatilia jambo hili baada ya kurudi, nimepata taarifa kidogo za mkanganyiko na

sasa hivi tunajaribu kutafuta suluhu ya jambo hili. Kilichotokea ni nini? Nimeelezwa kwamba, Marekebisho ya Sheria ambayo yalipitishwa na Bunge hili, nadhani mwaka 2009/2010, inasemekana kwamba, yalibadili kabisa kilichokuwepo katika sheria iliyokuwepo awali ambayo ilikuwa inapiga marufuku uuzaji wa kahawa mbichi au ununuzi wa kahawa mbichi.

Zipo Kanuni ambazo zimetengenezwa kutokana na mabadiliko hayo, ambazo zinaruhusu uuzaji wa kahawa hiyo ambayo haikukobolewa. Nimewaambia wataalam wangu wajaribu kutafuta hiyo sheria tuone kama kweli tulipitisha hivyo, kwa sababu si kwa maslahi ya mkulima mdogo hata kidogo. Nikasema nitashangaa sana kama lilitupita na halikuwa na mjadala mkali hapa kwa sababu kwa vyovyote vile suala la kuongeza thamani ya zao ndiyo kila Mbunge hapa angependa ifanyike katika kila zao. Imekuwaje katika hili tukakubali. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Zambi kwamba, jambo hili lazima tulipatie ufumbuzi wa haraka.

Sasa ni kweli niliwaambia wazungumze kwani nilijua kabisa kwamba, matokeo yake yatakuwa ni yale kwamba Sheria inasema hivi. Baada ya kupewa huo mkanganyiko, basi tunali-*sort out* na wenzetu wa Wizara ya Sheria, tutarudi tena kuja kueleza ukweli wa jambo hili na hatua stahiki zitachukuliwa. Nataka nimuahidi Mheshimiwa Zambi kuwa, hili jambo tunalipa umuhimu mkubwa, tutaharakisha sana kupata Sheria hizo zote na tuweze kuzichambua na kuona kilitokea nini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru kwa majibu yako mazuri sana. Simu ninazopata hivi sasa kutoka kwa Wananchi wa Mbozi na maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya na nilikuwa nazungumza na Wabunge wenzangu wa Mbeya Vijijini na Ileje, wanasema kwamba, wizi mashambani unaendelea kwani vijana wanaenda kuchuma kahawa au wanakata miti ili wapate kahawa chapu chapu, hiyo *red cherry,* wanaenda kuiuza.

Serikali haioni umuhimu kupiga marufuku au kusimamisha zoezi hilo mpaka hapo utakapopata hizo Kanuni na kuzifanyia uamuzi? (*Makofi*)

**SPIKA**: Na wewe umeitisha mkutano saa saba wa wanaolima kahawa wote. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na rai ya Mheshimiwa Zambi, lakini kama nilivyosema, unapokuwa na Sheria inasema hivi; maana ninachoweza kupiga marufuku sidhani kama kitatekelezeka kwamba ninyi watu mnaokwenda kuiba na kupora kahawa kule mashambani acheni. Kama jambo lenyewe la msingi halijapatiwa ufumbuzi, kazi hiyo ni ngumu sana kwa sababu inahusu maeneo ambayo wakati mwingine hayatafikika. Bado naweza nikasema kwa ujumla tu kwamba, tuombe Vyombo vya Dola chini ya Mkuu wa Mkoa, kama wapo watu wanakwenda kuiba kwenye mashamba *fine,* hatua stahiki zichukuliwe, lakini mimi nadhani msingi mkubwa ni ku-*deal* na suala lenyewe la Sheria.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge Kijana.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Waziri Mkuu ni Kiongozi mkubwa sana Serikalini na kauli ya Waziri Mkuu ni kauli ya Serikali. Wakati wa mazishi ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo langu la Arumeru Mashariki, Mheshimiwa sana Jeremiah Solomon Sumari, Serikali kupitia Waziri Mkuu, ilitoa tamko kwamba, itahakikisha ahadi zote ambazo zilikuwa zimeahidiwa, itakwenda kuzitekeleza ndani ya *term* hii.

Kwa kuwa Mbunge ameshapatikana na ni Mbunge wa Wananchi; na kwa kuwa ahadi ya Waziri Mkuu ilikuwa ni ahadi kwa Wananchi. Je, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ipo tayari ili sasa nimletee ahadi zote ambazo zilikuwa zimeahidiwa kwa ajili ya utekelezaji ili isionekane kwamba ilikuwa ni kauli ya kisiasa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tatizo la vijana wangu, maana anaposema anafoka, unaona anatikisika kabisa kabisa. Hakuna sababu, lakini nimemwelewa anachosema ni nini. Mheshimiwa Nassari, tulichokisema pale, tulikuwa tunazungumzia ahadi zinazotokana na Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi; ni wajibu wetu kama Serikali kwa kile kilichoelezwa katika Ilani hiyo na hata yale yanayotokana na kauli za Viongozi kwa nyakati tofauti. Tumekuwa tukisema tutajitahidi kuzitekeleza. Kwa hiyo,

nataka nirudie, tutazitekeleza kwa sababu ndiyo ahadi ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali langu linalenga yale yale ambayo yaliahidiwa kwenye Ilani hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu yaliahidiwa na Mbunge wa Chama cha Mapinduzi. Ninauliza kama Serikali ipo tayari kuyatekeleza. Swali langu la msingi lilikuwa ni yuko tayari nimletee sasa ili ayatekeleze kwa sababu ninayafahamu kuliko anavyoyafahamu yeye; kwa sababu mimi nilikuwa mwananchi wa Mbunge yule? Kwa mfano, tatizo la ardhi ambalo limekuwepo tangu ukoloni mpaka leo hii, ambalo limepelekea mpaka vifoo vya watu hivi karibuni. Je, Serikali inatoa kauli gani kwamba ipo tayari sasa kushughulikia tatizo hili ili Wananchi wa Arumeru Mashariki waondoke kwenye migogoro na wasiedelee kufa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kama Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imesema inaahidi kutatua migogoro kwenye Jimbo la Mheshimiwa Nassari, lakini migogoro yoyote ni sehemu ya uendeshaji wa shughuli za nchi. Kwa hiyo, mahali popote kunapotokea mgogoro, wajibu wetu ni kuhakikisha tunatanzua ule mgogoro. Migogoro ya ardhi popote imekuwa inashughulikiwa. Kwa hiyo, hata kama Nassari una mgogoro wa ardhi, bado Serikali italishughulikia. Rai yangu kwa Viongozi ni kuacha kutumia nafasi zetu hizi kwa namna moja au nyingine kuwa sehemu ya uchochezi wa migogoro hiyo, maana mengine ni yetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana, tupo tayari na tutafanya kazi hiyo kwa imani kubwa kabisa, ila na sisi Viongozi tusaidie, badala ya kuwa sehemu ya tatizo ambalo linajitokeza. *(Makofi)*

**MHE. AHMED ALI SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kutokana na hali ya tatizo la njaa ambalo bado linaendelea kwenye maeneo mengi nchini Tanzania ikiwemo Mkoa wa Shinyanga na hasa Jimbo la Solwa, mwaka jana ilifanyika tathmini kati ya mwezi wa tatu mpaka mwezi wa tano, chakula kikapelekwa kwenye maeneo hayo yote, lakini kwa bahati mbaya sana chakula chenyewe nacho kilichukua zaidi ya miezi minane kuwafikia Wananchi.

Vile vile baada ya Serikali kuhisi kwamba tathmini ile ilikosewa kwa maana ukilinganisha na 2006, tofauti ilikuwa kubwa sana, Serikali ilifanya tathmini nyingine tena mwezi wa saba. Kutokana na hali mbaya ya hewa, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama mtoto wa mkulima unaelewa, ulikuja Mkoa wa Shinyanga na maeneo mengine unafahamu hali ilivyokuwa. Kutokana na tathmini iliyofanyika mwezi wa saba kuhusu suala hili; ni lini Serikali itatoa tamko ili Wananchi wawe na matumaini kwa Serikali yao waliyoichagua kuondoa adha hii ya njaa ambayo wanayo mpaka sasa hivi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tumekuwa na tatizo hili la ukame katika baadhi ya maeneo hasa Mkoa wa Shinyanga na kiasi fulani na Simiyu. Zipo pia Wilaya nyingine nyingi ambazo

zilikumbwa na tatizo hili na tumekuwa tunalishughulikia karibu muda wote. Tatizo lililotokea kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga ni kwamba, chanzo chao kikubwa cha chakula kinatoka Mkoani Rukwa na njia pekee ya kusafirisha mazao yale ni reli kutoka Mpanda mpaka Tabora na kutoka pale wanasafirisha kwa reli tena kuelekea Shinyanga. Kwa kipindi kirefu kidogo tumekuwa na tatizo hilo la mabehewa kutoka Wilayani Mpanda, jambo ambalo limeathiri sana usambazaji wa chakula katika maeneo yenye shida.

Nataka nikuahidi Mheshimiwa Salum kwamba, jambo hili tunalifahamu na tunalishughulikia sana, tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu wote kuhakikisha kwamba, tunapeleka chakula. Hivi sasa hali siyo mbaya sana kwa maana ya usafirishaji, kwa sababu hata barabara kiasi fulani zinapitika. Kwa hiyo, tunajipanga kuhakikisha kwamba tunapeleka chakula kwenye maeneo hayo mapema iwezekanavyo.

**MHE. AHMED ALI SALUM:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yako mazuri na yenye matumaini.

Sasa ili tatizo hili la ucheleweshaji wa kupeleka vyakula hivi kwenye maeneo haya lisitokee kama ilivyokuwa hapo nyuma; Mheshimiwa Waziri Mkuu unawaahidi nini Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, Jimbo la Solwa na maeneo mengine yote kwamba chakula kitaletwa lini na haraka iwezekanavyo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, *of course,* ukisema kinaletwa lini, sina jibu ndiyo maana

nimekuahidi tu kwamba, kwa sababu tunaosimamia zoezi hili ni Ofisi ya Waziri Mkuu, ndiyo tunaohangaika na jambo hili, tunalifahamu na tunajua kitu gani kilitokea kilichosababisha hatua hiyo kukwama. Kwa hiyo, nimekwambia hapa kwamba, tunafanya juhudi kubwa sana kuhamisha chakula pale Mpanda kiliporundikana kukipeleka Shinyanga, kwa sababu sasa angalau hali ya mvua imeshakwisha. Kwa hiyo, tuna uwezo mkubwa zaidi kidogo wa magari, lakini reli nayo sasa inafanya kazi kwa kiwango fulani; hivyo, nayo hiyo tutaitumia.

Ninataka niseme lingine ambalo nililisema nilipokuwa ziarani Shinyanga. Nilisema, nawaomba sana Viongozi wa Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na maeneo mengine yenye matatizo ya ukame, tusitegemee muda wote kwamba chakula lazima kiwe ni kile kinachotokana na juhudi za Ofisi ya Waziri Mkuu. Niliwapa changamoto kwamba, nilipopita maeneo mengi, nimekuta wana mifugo mingi, Shinyanga kuna ng'ombe wengi sana; nikawasihi sana kwamba, wazungumze na Mikoa hii inayozalisha, watafute utaratibu wa kuweza kusaidiana kupata wafanyabisahara huko huko au kutafuta utaratibu utakaotuwezesha kupata chakula hiki kutoka Mikoa hiyo kwa kubadilishana tu na ng'ombe ambao wako pale kwa wingi. Niliwaambia ng'ombe mmoja hutakosa laki tatu na nusu. Nikasema kwa ng'ombe mmoja huyo laki tatu na nusu, una magunia kumi ya mahindi kutoka Mkoani.

Sasa hili ni jambo ambalo linawezekana kabisa na nikasema tukijipanga tunaweza. Kwa hiyo, matumaini

yangu ni kwamba, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Rukwa na Katavi, mazungumzo haya yangeanza mapema kwa sababu ni kitu tunachoweza kuepusha. Unajua mimi naona kunakuwa na aibu lakini rasilimali ya kuweza kutoka pale tunayo na mifugo inaweza ikawa ni suluhu moja rahisi sana.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Katika nchi yetu kumekuwepo na migogoro mikubwa ya ardhi na mingi inasababishwa na Serikali au makampuni fulani kupita katika maeneo ya Wananchi na kutathmini ardhi yao kama ilivyokuwa katika Jiji la Dar es Salaam na Mikoa mingine. Kwa mfano, mwezi Agosti, 2011 Kampuni ya *Kilwa Energy* kwa niaba ya *SONGAS* ilipita maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam yakiwepo maeneo ya Kivule, Guruka kwa Lala, Ulongoni na kadhalika, kwa ajili ya kutathmini maeneo mbalimbali ya Wananchi ili waweze kuendeleza shughuli zao wenyewe. Kuanzia wakati huo, waliwaahidi Wananchi kwamba miezi mitatu tu wangelipwa fedha zao. Sasa ni takriban mwaka mmoja hawajarudi kuwaambia chochote Wananchi na hawajalipwa na Wananchi wamesitisha…

**SPIKA**: Naomba usifanye hotuba sasa.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, Wananchi wamesitisha shughuli zao za maendeleo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuingilia kati suala hili ili

Wananchi hawa walipwe au waruhusiwe kuendelea na shughuli zao za kiuchumi?

**SPIKA:** Ni masuala ya fidia tu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Eugen Mwaiposa swali lake zuri kwa maelezo yafuatayo:-

Kwa upande wa eneo la Ukonga, ni kweli kwamba tunayo Miradi miwili pale ambayo inaendelea na yote inahusisha upitishaji ama wa bomba au *transmission* kwa ajili ya umeme. Miradi yote miwili ina mambo makubwa mawili; moja ni tathmini ya kimazingira katika eneo linalopitisha miundombinu hiyo. Ya pili, ni ridhaa kutoka Wizara ya Ardhi kuhusiana na masuala hayo ya fidia, maana ikishafanyiwa tathmini ni lazima Wizara ya Ardhi nayo ijiridhishe kwamba tathmini ile ni sahihi na imezingatia vigezo vya kisheria. Kwa hiyo, katika maeneo haya mawili kumekuwa kidogo na kuchelewa, lakini tunalifuatilia na mimi nataka nikuahidi dada yangu kwamba, nitajitahidi mimi mwenyewe kuzungumza na Waziri wa Ardhi tuone kama lile tatizo limekwisha. Upande mwingine ni *NEMC,* ambao ndiyo wanashikilia kile kibali, tukisha-*clear* hiyo basi suala la malipo litafuata. Kweli ni jambo ambalo linachukua muda kidogo, lakini tulichelewa kwa sababu hiyo tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa majibu mazuri kwa maswali mazito. *(Makofi)*

Ninawashukuru pia Wabunge kwa kuweza kujitahidi kuuliza maswali ya Sera na kwa kuwa majibu yalikuwa marefu, tumewakosa watu wawili kumalizia. Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu hatua inayofuata.

## MASWALI YA KAWAIDA

Na. 53

### Matumizi ya Dawa za Kulevya kwa Vijana

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Nchi yetu imekumbwa na balaa la vijana kujiingiza katika matumizi ya madawa ya kulevya na kuathiri nguvu kazi ya Taifa:-

Je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya kadhia hiyo ambayo inaendelea kwa kiasi kikubwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kukabiliana na athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana:-

(i) Kutoa elimu kwa vijana, familia, waelimishaji na jamii yote kupitia vyombo vya habari, michezo ya

kuigiza na matukio maalum ya Kitaifa na kuanza kuingiza somo la madhara ya dawa za kulevya katika mitaala ya elimu;

(ii) Kulifanya suala la dawa za kulevya na UKIMWI kama Kaulimbiu ya kudumu katika Mbio za Mwenge wa Uhuru hata mwaka huu;

(iii) Kwa kushirikiana na wadau wengine, Serikali imeanzisha huduma rafiki kwa vijana kusaidia kuacha matumizi ya dawa za kulevya bila kutumia dawa na kujenga kituo cha tiba na utengamao kilichopo Itega karibu na Taasisi ya Isanga, Dodoma; na

(iv) Kutoa tiba ya bure kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya katika Hospitali za Afya ya Akili na dawa za kulevya zilizopo nchini na kuwekea mkazo suala la ajira kwa vijana ili wajishughulishe zaidi na shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali pia ipo katika harakati na mchakato wa kuunda chombo madhubuti zaidi cha kudhibiti dawa za kulevya na kutunga Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na kuipitia Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 1995. Napenda nitoe wito kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, kutoa ushirikiano wa dhati katika jitihada za Serikali za kukabiliana na tatizo hili.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Suala la madawa ya kulevya linatokana zaidi na waingizaji wakubwa wa madawa haya. Je, ni kwa nini sasa wakati wanapokamatwa inachukua muda mrefu sana kumaliza kesi zao wakati ushahidi unakuwa ni wa *ready-handed?*

(ii) Je, ni kesi ngapi zinazohusiana na madawa ya kulevya ambazo zimeshatolewa hukumu na ni ngapi bado hazijasikilizwa?

**SPIKA:** Swali la pili ni kazi kweli. Haya Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tatizo hili ni kubwa na kama anavyosema, wapo wasafirishaji wakubwa wanaohusika na biashara hizi. Labda niseme kwamba, kuanzia Januari mpaka Mei mwaka huu, gramu laki mbili na thelathini nukta tisa za *heroin* na gramu 16,000 za *cocaine* zilikamatwa. Watanzania wengi walikuwa wanajihusisha na biashara hizi; kwa mfano, mwaka 2005 na 2010, Watanzania 211 walikamatwa nje ya nchi, ambapo miongoni mwao wamenyongwa kulingana na Sheria ambazo zinatawala maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa ufupi na nikiri kwamba, kesi hizi zinachukua muda mrefu sana na hilo

alilosema, kwa mujibu wa Sheria ya sasa, hata mtu akikamatwa na *red cherry* na dawa za kulevya zile, bado siyo ushahidi wa kutosha. Kesi itaendelea kusikilizwa na dawa zile zitaendelea kupelekwa Mahakani kama kidhibiti, mpaka kesi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema hapa kwa ufupi kukatisha majibu ya swali hili. Jambo hilo tumeliona wazi na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, anajua jambo hilo na ndiyo maana tunafanya mapitio ya Sera na Sheria *comprehensively* ili angalau kuziba mianya hiyo. Ifikie mahali kwamba, mtu akikamatwa na dawa za kulevya sasa hivi, basi hizo dawa iwe kielelezo moja kwa moja badala ya kusubiri hizo dawa ziwe zinaoneshwa Mahakamani kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa, jambo hilo linajulikana; pamoja na ucheleweshwaji wa kesi, zipo sababu nyingi sana na *technicalities* nyingi sana za Kisheria ambazo sasa Serikali imeamua kuziba mianya hiyo.

**SPIKA:** Subiri hiyo kesi mapema. Sasa twende Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Jerome Bwanausi, atauliza swali hilo.

Na. 54

**Fedha za Kumalizia Kituo cha Afya Lupaso**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kutenga fedha za kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Lupaso katika Mwaka wa Fedha 2011/2012:-

(b) Je kwa nini fedha hizo hazijapatikana hadi sasa?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Wananchi wa Jimbo la Lulindi kuhusu umaliziaji wa Kituo ulioahidiwa tangu mwaka 2006?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, kutoka Jimbo la Lulindi, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilikamilisha kazi ya ujenzi wa majengo mbalimbali na miundombinu katika Kituo cha Afya Lupaso, kwa kiwango cha kuweza kutumika. Serikali ilikuwa imeshamlipa Mkandarasi, *M/S BM Construction Co. Ltd,* kiasi cha shilingi 685,025,504.00 kwa kiwango cha kazi iliyokuwa imekamilika. Kitengo cha Majengo cha Wizara kilishirikiana na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa ushauri uelekezi wa Mradi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba, Kituo cha Afya cha Lupaso kinahitaji kukamilisha zoezi la upatikanaji wa maji, umeme, watumishi, vifaa na

vifaa tiba ili kiweze kuanza kutoa huduma za tiba. Serikali kupitia Wizara inaagiza mambo yafuatayo yaweze kufanyika:-

(i) Wizara yangu kupitia Kitengo cha Majengo, Mkandarasi aliyekuwa anajenga kituo hicho na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, wakae pamoja na watatue matatizo madogo madogo ili wakabidhi majengo na kuwezesha utoaji wa huduma katika Kituo hicho kuanza mara moja;

(ii) Wizara na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, kwa pamoja zikamilishe zoezi la upatikanaji wa maji na umeme mara moja;

(iii) Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ipeleke watumishi, vifaa na vifaa tiba vinavyotakiwa katika Kituo cha Afya cha Lupaso ili kukiwezesha kituo kianze kutoa huduma ikiwa ni pamoja na upasuaji mkubwa; na

(iv) Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ijumuishe Kituo cha Afya cha Lupaso katika orodha ya Vituo vinavyopatiwa dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya Dawa *(MSD)*.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa shilingi milioni 835 kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hiki; na kwa kuwa fedha zilizotolewa na Serikali kulingana na majibu ya

Mheshimiwa Waziri ni shilingi milioni 685. Kwa kuwa ahadi hii ni ya tangu mwaka 2006 na sasa ni mwaka 2012; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwahakikishia Wananchi wa Jimbo la Lulindi kwamba maelezo ya ahadi anazozitoa ni utekelezaji wa suala hili katika kipindi cha mwaka 2012/2013?

(ii) Kwa kuwa kwenye jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea umuhimu wa kuwa na vifaa pamoja na watumishi katika Hospitali ya/au Kituo cha Lupaso. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza akalihakikishia Bunge na Wananchi wa Lulindi kwamba upo mkakati wa dhati wa kuhakikisha kwamba vifaa hivi na watumishi wanapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jerome Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala linalotakiwa ni kuhakikisha kwamba, Kituo cha Lupaso, kinakamilika na kinaanza kazi mara moja. Hatua hizo tumeshazieleza na nitasimamia kuhakikisha kwamba, zinatekelezeka kwa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni la vifaa kupelekwa na watumishi; limo katika jibu langu la msingi. Kwa hakika kuhusu suala la vifaa ni baadhi tu ya vifaa ambavyo vimepungua siyo vyote, karibu vifaa vingi vipo. Kuna baadhi tu ya seti ambazo zimepungua na siyo zote na nimethibitishiwa kwamba, zitaweza kupelekwa kwenye Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, watumishi tayari wapo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na baadhi yao watakuwa tayari kuhamishwa kupelekwa katika Kituo ili waweze kuanza kazi.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumetokea mabadiliko ya Mawaziri na ninaamini Waziri hakupata nafasi ya kufika Masasi na kukiona Kituo hiki. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda Masasi, Jimbo la Lulindi, kwenye Kituo cha Afya hiki cha Lupaso, ukajionee wewe mwenyewe jinsi Serikali ilivyowekeza majengo ambayo Mheshimiwa Rais alishafika pale na kufanya uzinduzi ambao kumbe alikuwa anadanganywa na sasa ni mwaka wa sita hakifanyi kazi Kituo hiki ili uweze kupata fursa ya kukaa na Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuona ni kipi Halmashauri yetu inaweza ikasaidia katika kukamilisha na mzigo upi ubebe Wizara? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba, mimi au Wizara yangu itakuwa tayari kwenda kutembelea; ninaahidi baada ya kukamilisha Bunge, nafikiri ninaweza nikaenda kutembelea.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwa kuwa Mkoa wa

Mtwara una Kata 149 na Vijiji 738; na kwa kuwa huduma hii ya afya katika Mkoa mzima wa Mtwara ikiweko Lupaso, kuna zahanati 160 tu. Je, Wizara ya Afya haioni kuna umuhimu wa kuhakikisha rasilimali zinazopatikana Mkoani Mtwara angalau asilimia 30 inabaki kwa ajili ya kukuza huduma ya afya katika Mkoa mzima wa Mtwara likiwemo tatizo lililoko katika Kata ya Lupaso, Jimbo la Lulindi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimwia Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la msingi linazungumzia Kituo cha Afya cha Lupaso na swali lililoulizwa linazungumzia Vituo vya Afya vyote na suala la kubakiza mapato katika Halmashauri. Kwa hakika, mapato yote ambayo yanapatikana katika Vituo vya Afya, huwa yanabaki katika Vituo husika na Halmashauri husika; ni suala la Halmashauri kutumia mapato hayo yanayopatikana katika vituo kwa ajili ya maendeleo na sehemu kubwa tunawashauri waitumie kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa dawa. *(Makofi)*

Na. 55

**Shamba la Mkonge la Ndungu Kurudishwa kwa Wananchi**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Jimbo la Same Mashariki lina Shamba la Mkonge lenye takriban hekta 1,231 alilokabidhiwa Mwekezaji *(L. M. Investment)* tangu mwaka 1998 kwa lengo la kuwekeza katika Kilimo cha Mkonge, jambo ambalo siyo linalofanyika kwa sasa:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kurejesha ardhi hiyo kwa Wananchi wa Kata ya Ndungu ambao kwa sasa wana uhaba mkubwa wa ardhi ya kilimo na makazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Ndungu, lenye ukubwa wa hekta 1,230.9 lilibinafsishwa mwaka 1997 kwa Kampuni ya *L M. Investments,* likiwa kwenye hali mbaya ya vichaka, mfereji wa maji ulikuwa umeharibika, korona na kayamba zilikuwa mbovu baada ya kuhujumiwa na watu wasiojulikana. Aidha, matrekta yalikuwa mabovu na nyumba za wafanyakazi zilikuwa zimebomoka na hivyo uzalishaji kwenye shamba ulishasimama. Wakati shamba hili linabinafsishwa, lilikuwa ni mali ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania *(TSA).*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya mwekezaji kuchukua Shamba hili, alifanya juhudi za kulifufua kwa

kukarabati miundombinu ikiwemo korona, mfereji wa maji, nyumba za wafanyakazi na kujenga nyumba mbili mpya. Pia, ameboresha mitambo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji *(Hydro-Power),* kukarabati matrekta yaliyokuwepo na kununua mapya mawili. Pamoja na hayo, jumla ya hekta 647 zimeshapandwa mkonge na kati ya hizo, hekta 545 zipo tayari kuvunwa na hekta 102 zina mkonge mdogo na ameshaandaa hekta 250 kwa ajili ya kupanda mkonge mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji ameajiri takriban wafanyakazi 200, ambapo kati ya hao, 112 ni wafanyakazi wa kudumu na wanaobaki ni wa msimu, kutokana na kazi zinavyojitokeza; mfano, kulima, kupanda na kusafisha mkonge. Uzalishaji kwa kipindi cha miaka mitatu (2009 – 2011) ni wastani wa tani 14 za singa kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2012, Wizara yangu iliunda kikosi kazi kufuatilia na kujiridhisha juu ya hali ya Zao la Mkonge nchini na mashamba yaliyobinafsishwa; na kwenye ripoti yake imeonesha kujiridhisha na jitihada za mwekezaji kuendeleza Shamba la Ndungu, hususan kwenye maeneo ya uzalishaji, ajira na uwekezaji. Serikali inaona mwekezaji apewe nafasi ya kuendelea kuboresha Shamba hili. Hata hivyo, maamuzi ya kurejesha ardhi ya Shamba hilo kwa Wananchi wa Kata ya Ndungu, yanaweza kufanyika kama Mwekezaji atakuwa amekiuka makubaliano ya awali ya Kimkataba, yaliyofikiwa wakati wa kuingia Mkataba huo. Aidha, uwekezaji huu unahamasishwa kuzingatia pia manufaa mapana

yanayopatikana kwa wakazi wanaozunguka maeneo ya mashamba haya. Pia, uwekezaji huu unapofanywa na Wazalendo kama ilivyo kwenye Shamba la Ndungu, Serikali inahamasika na kusisitiza ushirikiano wa wadau wote.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, *in a very serious note,* ninasikitishwa na Serikali kuingia kwenye malumbano na Mbunge wa Jimbo.

(i) Kwa kuwa sasa hivi ninapoongea hapa Shamba hili la Ndungu, Mwekezaji huyu ana sehemu kubwa ameikodisha kwa kilimo cha tangawizi na ameharibu skimu ya umwagiliaji ambayo ni *grant* tumepewa na Wajapani. Mimi ndiyo mwenye Jimbo lile na ninayaelewa. Je, Serikali haioni kwamba hainitendei haki kwa kutoa jibu ambalo siyo sahihi na itabidi iende ikaone uharibifu ule na ije iniombe radhi hapa ndani?

(ii) Kwa kuwa katika jibu la Mheshimiwa Waziri anasema wameunda Kikosi Kazi; mimi nasema Kikosi Kazi hiki kimetoa majibu ambayo siyo sahihi. Je, Serikali hamwoni kuna umuhimu sasa wa kuunda Kikosi Kazi ambacho kitatujumuisha na sisi Wabunge wenye matatizo hayo ya Wawekezaji wa Mkonge ambao wanawadhulumu Wananchi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Naibu Waziri, kwa sababu ameingia muda mfupi, lakini amekuwa anajitahidi kuanza kuelewa shughuli zinavyoendelea kwa muda mfupi. Pia naomba niseme kwamba,

tumepitia Taarifa ya Kikosi Kazi ambacho kimetembelea mashamba haya; kwanza hakijamaliza kazi yote, kimefanya nusu. Tulipokuwa tunaangalia, bado katika hadidu za rejea pia kuna mambo ambayo yanakamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimuahidi kabisa Mheshimiwa Anne Kilango kwamba, tutakwenda kuangalia kazi iliyokwishafanyika na hasa migogoro ambayo ipo, ambayo inahusisha matumizi tofauti na yaliyokuwa yamekusudiwa, ambayo yameingiliana pia na wakulima wa tangawizi na migogoro ya maji ambayo imejitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Anne Kilango kwamba, suala hili mimi mwenyewe nimeliona. Tutakwenda, kulitazama upya na tutashirikiana na yeye ili tulipatie majibu sahihi. *(Makofi)*

Na. 56

**Usalama wa Mipaka ya Nchi za Afrika Mashariki**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Kwa kuzingatia manufaa na faida za ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa mipaka ya nchi yetu na raia wake:-

(a) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani unaoshirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na ile ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuepuka tofauti

za kiutendaji zinazoweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu?

(b) Je, Tanzania Visiwani inapata ulinzi madhubuti kwenye mipaka gani kama ilivyo katika mipaka ya Tanzania Bara na Nchi nyingine za Afrika Mashariki?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi, suala la usalama wa nchi yetu linawashirikisha wadau mbalimbali kama vile Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi na Uhamiaji, wanatekeleza majukumu yao ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana. Vyombo vya Ulinzi na Usalama, vinafanya kazi kwa kubadilishana Taarifa. Pale inapobidi, vinafanya operesheni za pamoja katika kulinda Ulinzi na Usalama wa nchi yetu. Katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, nao hukutana kujadili masuala mbalimbali ya Ulinzi na Usalama.

(b) Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere kuwa, Tanzania Zanzibar, kama ilivyo kwa sehemu nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inapata ulinzi madhubuti katika mipaka yake yote. Zanzibar inapata ulinzi

upande wa Kaskazini, ambako Tanzania inapakana na Kenya, Msumbiji na Comoro Kusini na nchi ya Shelisheli upande wa Mashariki. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, kwa kutumia Vikosi vyake; Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Anga na Wanamaji, vilivyopo Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara, linashirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuipatia Ulinzi wa kutosha Zanzibar.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (1) ya Katiba ya Zanzibar inasema, naomba ninukuu: *"Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyoizunguka na Bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar."*

(i) Kwa kuzingatia kwamba, Zanzibar ni nchi huru na kwa kuzingatia kwamba Uanachama wake katika Shirikisho la Afrika Mashariki unaegemea mgongoni kwa Tanzania Bara. Je, ni lini sasa Serikali itaunda Chombo Huru ambacho kitahakikisha kwamba Zanzibar inapata haki zake zote zitokanazo na Shirikisho la Jumuiya hii? *(Makofi)*

(ii) Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ushirikiano wa Afrika Mashariki haupo kwenye mambo ya Muungano. Je, ni jinsi gani sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa

stahiki zake kwa Zanzibar kikamilifu bila kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali limeanza ulinzi mpaka limekwenda wapi huko, haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kama alivyosema kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, eneo la Zanzibar ni sehemu yote ya Zanzibar yaani Unguja na Pemba na sehemu za bahari ambazo zinazunguka. Lakini hata ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza hivyo hivyo katika Ibara ya 2(1), inaeleza eneo la Tanzania Bara na inaeleza eneo la Zanzibar. Sasa lakini hili haliondoi ukweli kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Muungano ulioasisiwa mwaka 1964. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Zanzibar hata ukiangalia Ibara ya 102(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambapo sote tunapaswa kuiheshimu, inatambua mipaka ya Zanzibar na inatambua kuwepo kwa Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maana hiyo basi, kama Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 102(1) sioni kama kuna hoja ya msingi ya kuunda chombo maalum ambacho kitasimamia maslahi ya Zanzibar kwa sababu, kwanza tumekubali kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia katika ushirikiano wa Afrika Mashariki tunatambua yako mambo ambayo si ya Zanzibar na hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

inatambua hivyo, kwamba yako masuala ambayo ni ya Zanzibar pekee.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa utaratibu ambao tunatumia na tukaelewa kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaposhirikiana na nchi nyingine nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania masuala yote yanasimamiwa chini ya utaratibu ama Wizara ya Mambo ya Nje au kwa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ndiyo ambayo inaratibu masuala yote hayo na kwa maana hiyo basi kumekuweko na vikao mbalimbali ambavyo vinahusiana na masuala mbalimbali yanayojadiliwa katika Afrika Mashariki.

Kwa yale mambo ambayo Zanzibar inataka ushiriki wake au hoja zake ziweze kuelezwa vizuri basi kumekuwa na ushirika wa watendaji kwa upande wa Zanzibar ambao wanatoa maoni yao wakishirikiana na wenzao wa Tanzania Bara kwa pamoja kuandaa mikakati ya pamoja na kuandaa hoja ya pamoja ambayo baadaye inawasilishwa katika vikao mbalimbali vya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kwa mnasaba huo basi sioni kwamba kuna hoja ya msingi sasa ya kuunda chombo maalum kwa ajili ya kushughulikia maslahi ya Zanzibar kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muwe mnaangalia na saa, saa imepita lakini nina swali moja lazima liulizwe kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Rita Mlaki atauliza swali hilo.

Na. 57

## Mauzo ya Nje na Kupanda kwa Thamani ya Shilingi

**MHE. RITA L. MLAKI** aliuliza:-

Kipindi cha hivi karibuni thamani ya shilingi imeshuka sana na kuathiri uchumi wa nchi na maisha ya Watanzania kutokana na kuwa nchi yetu haina mauzo ya nje:-

(a) Je, Serikali, inajua kuwa thamani ya shilingi itapanda iwapo tutaongeza kuuza bidhaa zetu nje?

(b) Je, Serikali, imewawezeshaje Wawekezaji wa ndani na nje kuuza bidhaa zao nje?

(c) Je, Serikali, inajua ni bidhaa gani za kilimo zimepelekwa nje na kiasi gani za kilimo zimepelekwa nje na kisi gani cha fedha kimepatikana?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, thamani ya shilingi itapanda endapo tutaongeza kuuza bidhaa zetu nje. Hii itategemea kama tutaongeza uzalishaji wa bidhaa

na huduma kwa kiasi kikubwa kukidhi soko la ndani na baadaye ziada ziuzwe nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje kuuza bidhaa zao nje kwa kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji yaani *(EPZA),* kwa kutenga na kuendelea kuwatengea wawekezaji maeneo ya uzalishaji katika mikoa yote nchini. Aidha, tangu kuanzishwa kwa Mpango wa *EPZ* mwaka 2002 hadi hivi sasa 2012, jumla ya makampuni 40 kati ya makampuni 54 ya ndani na nje ya nchi, yamekuwa yakizalisha kwa utaratibu uliowekwa na Mamlaka ya *EPZ A.*

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na maonesho ya Saba Saba, Nane Nane na Maonesho ya Kikanda, yanayosimamiwa na kuratibiwa na *SIDO,* ambayo hufanyika kila mwaka yenye lengo la kuwapa fursa wafanyabiashara wetu kutangaza na kupata masoko ya kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa toka Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato kwa kipindi cha mwaka 2007 - 2011, bidhaa za kilimo zinazouzwa nje ni pamoja na Kahawa, Pamba, Katani, Chai, Tumbaku, Korosho na Karafuu. Mpaka sasa thamani ya bidhaa zilizouzwa nje ya nchi imeongezeka kutoka Shilingi Milioni 410,095 mwaka 2007 hadi Shilingi Milioni 1,079,007 mwaka 2011.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri hasa kukubali

kwamba thamani ya shilingi itaongezeka iwapo tutauza bidhaa nje. Hata hivyo, napenda kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

Pamoja na uanzishwaji wa *EPZ* ambayo kwa sasa anasema ina viwanda 54 na bado haijaenea nchi nzima na pamoja na Maonesho ya Saba Saba, Nane Nane, bado thamani ya shilingi yetu inayumba. Je, Serikali haioni umefika wakati muafaka sasa kufanya juhudi madhubuti kabisa za kusaidia wafanyabiashara kujenga viwanda vikubwa ili tuweze kuuza bidhaa nje?

Mheshimiwa Spika, la pili, pamoja na Serikali kuuza bidhaa nje tumeona zote ni *cash crop* lakini pia kuna masoko ya *European Union, EBA Everything But Arms* na ya America, *AGOA*, ambayo nchi yetu bado haijajumuika kwa kiwango kikubwa. Je, Serikali inaweza ikatueleza imefanya mpango gani kuwasaidia wafanyabiashara ili waweze kuingia katika masoko hayo na kuuza bidhaa zingine za kilimo, zikiwemo mboga, nguo na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naelewa kwamba Mheshimiwa Mlaki yeye naweza kusema kwamba, ni Naibu Waziri wa Viwanda Mstaafu na ni mdau mkubwa kabisa katika viwanda na biashara. Kwa hiyo, masuala haya mawili ambayo ameuliza nikianza na lile la pili kwamba kuna masoko ya nje ambayo yanajumuisha umoja wa Ulaya, *AGOA* kwa maana ya Amerika ambayo yametoa fursa kwa Tanzania au wananchi wetu kuweza kuuza huko kwenye masoko hayo. Ni kweli kwamba fursa hiyo ipo ya kuuza uko nje,

lakini liko tatizo kubwa sana ambalo kwa kweli nchi yetu kwa kiasi kikubwa imeshindwa kuuza nje kwa vile vikwazo ambavyo si vya kiushuru.

Kuna vikwazo ambavyo hawa wenzetu *AGOA* na Umoja wa Ulaya, *EBA* wameviweka, wametoa fursa lakini vikwazo ndiyo vinaleta shida, vile vikwazo ambavyo ni *non tax barrier*. Kwa mfano, hawa wenzetu wa *AGOA* na *EBA* wanataka hizo bidhaa zinazouzwa nje ziwe na ubora wa Kimataifa. Kwa hiyo, wametuwekea vikwazo kwamba wana *trace* mpaka huku tuliko ambako bidhaa hizo zinatoka, wana *trace back* mpaka wajue udongo uliotumiwa, mbolea iliyotumiwa iwe na ubora wa kiasi fulani. Kwa hiyo, vikwazo hivi vimetupa shida sana hapa Tanzania na kufanya kwamba Watanzania wetu washindwe kuuza bidhaa hizo nje kwa sababu ya vikwazo hivyo ingawaje kuna fursa hiyo. Kwa hiyo Serikali mpaka sasa inajitahidi kufanya mazungumzo na wahusika hawa ili waweze kulegeza masharti au vikwazo hivyo ambavyo wametuwekea ili tuweze kupata nafasi ya kuuza huko na kutumia hiyo fursa iliyoko.

La pili la kwamba, je, Serikali haioni kwamba viwanda hivyo 54 vilivyopo sasa hivi chini ya *EPZ* vimeshindwa au vinawezaje kuboresha thamani ya shilingi? Ni kweli kwamba viwanda vipo 54 au vimeanzishwa kati yao mpaka sasa hivi ninavyoongea, viko viwanda 40 ambavyo vimeonesha kwamba vinafanya vizuri na vinaweza kuongeza thamani ya shilingi. Vile vile mpaka sasa ninavyoongea, tumesikia hotuba ile ya hali ya uchumi ambayo imethibitisha kwamba kwa kiwango kikubwa *export* sasa

inaongezeka. Kwa hiyo, kwa kupitia hivi viwanda 40 ambavyo viko chini ya *EPZ* tunaweza tukaongeza *export.* Hivyo, jitihada kubwa ifanyike kwa hawa ambao wamepewa hii ikiwepo viwanda hivi 54 na vile 40 ambavyo vinafanya vizuri na sasa hivi kuongeza thamani ya shilingi inawezekana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na maswali yamekwisha. Nina wageni wafuatao:-

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao wanatoka *The East African* Nguvu Kazi *and Jua Kali Partners*, *where are they*? Wako pale wageni sikujua majina yao, lakini wanatoka kwenye *East African* Nguvu Kazi na Jua Kali *Partners*. Ahsante sana na karibuni, nadhani mtawaeleza watu hapa hicho kitu mnachokifanya huko.

Wageni wengine waliofika kwa ajili ya mafunzo, ni Waheshimiwa Madiwani 10 kutoka Halmashauri ya Serengeti. Madiwani kutoka Serengeti, karibuni sana na ahsanteni. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 54 kutoka shule ya msingi ya Chidachi, Dodoma, wanafunzi hawa na walimu wao walipo wasimame. Ahsante sana, tunawatakia msome vizuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na ya kwenu ninyi wenyewe.

Tuna wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Serikali Hombolo, Dodoma. Hawa naomba wasimame walipo. Kwa hiyo, hawa ndiyo wasomi wetu wa Serikali

za Mitaa baadaye, tunawatakia masomo mema na mfanye vizuri, matatizo katika sehemu ya maisha ni sehemu ya mpito, kwa hiyo yasiwafanye na nyie mkaacha kusoma. Karibuni sana.

Tuna wasanii 15 wa kikundi cha maigizo cha *Challenge Art Group* kilicho Makole, Dodoma. Wasanii hao wako 15, ahsanteni sana kwa ubunifu wenu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi; Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii saa saba mchana watakuwa na kikao kitakachofanyika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, sasa ana cheo gani? Lakini anaomba niwatangazie Wabunge wote wanaotoka maeneo yanayozalisha kahawa wakutane saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, kule kama mtagongana vyumba, basi mtawekana sawa kule kule.

Kuna tangazo la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe ambalo linahusu mabadiliko ya Baraza la Mawaziri na Wizara mpya. Kwa hiyo, Wizara Kivuli, kuna Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Kivuli ni Freeman Mbowe; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri mhusika ni David Ernest Silinde; kuna Wizara ya Miundombinu, Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Said Arfi na Naibu wake ni Pauline Gekul; yupo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Waziri Kivuli ni Profesa

Kulikoyela Kahigi; kuna Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango, Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Vile vile kuna Wizara ya Katiba Sheria na Muungano, Waziri wake Kivuli ni Mheshimiwa Tundu Lissu na ile ya Zitto Kabwe ya Uchumi na Fedha kuna Naibu Waziri Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai na kuna Wizara ya Maliasili, Utalii na Mazingira, Waziri wake kivuli ni Mchungaji Peter Msigwa; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wake Kivuli ni Vincent Nyerere; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Ezekia Wenje na Naibu wake Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Waziri wake kivuli ni Mchungaji Israel Natse; kuna Wizara ya Maji, Mifugo na Uvuvi, Waziri Kivuli wake ni Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi na yuko na Naibu wake Mheshimiwa Sabrina Hamza Sungura.

Pia ipo Wizara ya Kazi, Habari Utamaduni na Michezo, Waziri wake kivuli ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Naibu wake ni Mheshimiwa Cecila Pareso. Iko Wizara ya Nishati na Madini, Waziri Kivuli ni Mheshimiwa John Mnyika; Wizara ya Viwanda na Biashara, Waziri Kivuli wake ni Mheshimiwa Highness Kiwia; iko Wizara ya Afya, Jinsia na Jamii, Waziri Kivuli wake ni Dokta Antony Gervase Mbassa na Naibu wake ni Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Ipo pia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Waziri wake kivuli ni Mheshimiwa Susan Lyimo na Naibu wake ni Mheshimiwa Joshua Nasari. Ipo Wizara ya Kilimo na Ushirika, Waziri Kivuli wake anaitwa

Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na ipo Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi, Waziri kivuli wake ni Mheshimiwa Halima Mdee. Kwa hiyo, hilo ndiyo Baraza la Mawaziri Vivuli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, *concept* ya bajeti mbadala haipo kwenye kanuni, ila hayo wanayosema ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, tunaendelea, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011/2012 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na uchangiaji, sasa hivi nitamwita Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Abia Nyabakari na Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Moja kwa moja niseme kwamba, naunga mkono hoja ya Serikali ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa sababu Serikali ya CCM inafanya mambo mazuri ya

maendeleo na yanayoonekana na kuna mifano mingi nchi nzima. Mfano wa kwanza, nitoe kwenye Jimbo langu, Jimbo langu la Bukoba hivi sasa kuna mradi mkubwa wa umeme, unajengwa kwenda eneo la Ikimba *area*, vijiji zaidi ya 50 unafungwa umeme, umeanza mwaka jana na hivi leo umekamilika bado kidogo umeme uwake.

Miradi hii ipo sehemu mbalimbali nchini yaani miradi ya umeme, maji, barabara kwani hivi sasa kila mahali kuna Mkandarasi nchi nzima. Shule zinajengwa na zahanati pia, usalama wa nchi umeendelea kuwa imara, hii tumeizowea, tunaona ni kazi ya Mungu lakini siyo kazi ya Mungu pekee na pia Serikali ya CCM inafanya kazi. Kwa hiyo, naunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulipiga kelele sana humu ndani kuhusu kwamba, Serikali itie mkazo kwenye uboreshaji wa reli ili tunaokaa mikoa ya mbali na Dar es Salaam tupate huduma nzuri ya kupeleka bidhaa na abiria. Serikali ni sikivu, mwaka huu mmeona kwenye bajeti ilivyo reli imeongezewa mafungu makubwa. Kwa hiyo, nasema asiyeona haya ana matatizo makubwa ama ya macho au ya akili au vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo hapa kujadili bajeti hii ili kuboresha mipango hii ya bajeti ya maendeleo ili tupate maisha bora kwa kila Mtanzania. Kama nilivyosema Serikali inafanya vizuri lakini kuna watu ndani ya Serikali kwenye kutunga sera, watendaji wanaharibu mambo haya. Nina mifano, lakini muda hautoshi ila nitasema michache. Kwa mfano, kwangu

Bukoba Vijijini kuna kodi za adhabu sana kwani wananchi wanasumbuliwa sana na wananyanyaswa. Kodi za ushuru wa mazao, mtu anakwenda gulioni na ndizi moja kuuza ili anunue chumvi au mafuta ya taa. Bei ya ndizi ni shilingi 1,500/=, kabla hajafika sokoni njiani kuna *barriers* au vizuizi, barabara zote zimejaa vizuizi, kila kilomita tano au kumi kuna kizuizi. Anatozwa ushuru sh. 300/= au sh. 200/= kwa ndizi moja, akifika gulioni anaambiwa tena atoe ushuru mwingine sh. 300/= ndizi hiyo hiyo moja.

Mheshimiwa Spika, wananchi wananyanyasika na kusumbuliwa na huu ushuru ambao ni kinyume cha sheria. Sheria ya Kodi tuliyonayo inasema kima cha chini asitoe kodi, nafikiri leo ni sh. 140,000/=, mtumishi anayepata mshahara wa sh. 140,000/= hatozwi kodi, lakini mtu wa ndizi ya shilingi 1500/= anatozwa kodi. Hii kwa kweli sikubaliani nayo na naomba Serikali ichukue hatua ifute kodi hizi kwani hazina tija.

Mwaka huu Bukoba vijijini tuna bajeti nzima ya Halmashauri bilioni 26, ushuru wa kinyanyasaji na kikandamizaji ukitozwa kama ilivyopangwa ni milioni 21 sasa ni 21 kwenye bilioni 26 ni nini? Ni tone kwenye bahari. Kwa hiyo, hata mapato ya ushuru huu hayana tija kwenye Halmashauri, faida ya ushuru huu ni kusumbua wananchi tu peke yake. Kwa hiyo, naomba ushuru huu ufutwe ili wananchi wakae vizuri kwenye nchi yao na wafurahie kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nina lingine kule Bukoba, nina mradi wa Kabango *Bay*. Hii ni barabara kuanzia Mjini kwenda hadi Rubafu kilomita 42, pia inahusisha na

kujenga feri kuanzia inapoishia barabara kwenda mpaka nchi jirani ya Uganda. Mkataba ulisainiwa mwaka 2008, lakini hadi leo kazi haijaanza au haijafanyika, ni miaka mitano mkataba umesaini. Mwaka huu kwenye hiki kitabu cha bajeti kuna sh. 75,000,000/= kati ya thamani ya mkataba 46,000,000,000 sasa huku ni kukebehi wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Spika, barabara haiwezi kujengwa na ndiyo maana haijaanza kujenga kwani miaka mitano mkataba umesainiwa, mlisaini wa nini? Kama hakuna fedha mlisaini wa nini? Pia Serikali imejenga bandari ya uvuvi kubwa katika eneo la Malee, ni bandari kubwa sana na ya kisasa. Huwezi kubeba samaki 42 kwenye barabara ya vumbi, ikija mvua huendi samaki wanaoza, sasa tunavua samaki, hatuwapeleki kwenye Viwanda kule Kemondo. Sasa naomba barabara hii ijengwe.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mheshimiwa Magufuli alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi alikwenda kufungua ile bandari, akasema atamwomba Waziri wa Uchukuzi kwa vile mkataba ulishasainiwa barabara hii ijengwe, wananchi wakampigia makofi. Sasa funga fungua leo yeye ndiye Waziri wa Ujenzi, hajengi barabara hii wala haweki fedha kwenye bajeti. Hilo sikubaliani nalo ila bajeti hii nitaiunga mkono lakini bajeti ya ujenzi tutapambana, sitakubali, tutaikwamisha hadi tupate fedha kwenye barabara hii na ianze kujengwa angalau nusu kwenye mwaka huu na feri ijengwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kilimo. Bukoba kazi ya wananchi ni kilimo. Tunalima Ndizi ndiyo zao kuu na Kahawa na mazao mengine madogomadogo. Kwa sababu katika migomba ndiyo ndizi zinazalishwa limepigwa na ugonjwa unaitwa mnyauko au banana *wet*, hauna dawa. Mwaka jana 2011, mwezi Machi alikuja Waziri Mkuu akatupa pole tu na akahimiza watafiti waendelee na utafiti na watafute dawa pia alihimiza wananchi waendelee kulima kwa kutumia mbinu mbalimbali za kutoa ugonjwa huu. Sasa bahati nzuri mwezi Desemba mimi na Mheshimiwa Anne Tibaijuka ambaye ni Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Massawe tulikwenda Uganda kwa mwaliko wa Rais Museven, tukapata bahati ya kutembelea maeneo ya Kusini mwa Uganda kunakopakana na Bukoba wanakolima ndizi, tukaona wanavyopambana na ugonjwa wa mnyauko kwa mafanikio makubwa, mnyauko kweli upo, lakini huwezi kuuona wanajua namna ya kuudhibiti na ndizi zao hazina madhara.

Mheshimiwa Spika, sasa nikaja hapa nikamwomba Waziri wa Kilimo wakati huo na Naibu Waziri nikamweleza ilivyokuwa kule na nikamwambia naomba fedha kidogo milioni 30 au 40 ili nipeleke wakulima wa Bukoba kama 100 au 200 wajifunze kwa vitendo. Akasema hili ni jambo jema, akasema niandikie barua, nikamuandikia barua. Sasa hadi leo hata jibu hakuna, baadaye namsumbuasumbua hapa akanipa namba ya Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao. Nampigia simu anasema barua tumeipata tunaishughulikia, hakuna jibu mpaka leo na ndizi zinateketea kule. *(Makofi)*

Sasa ukiangalia bajeti ya kilimo kina kifungu kinaitwa *hospitality*, kina shilingi milioni 300, *hospitality* ndiyo nini? Kukirimu wageni, ndiyo maana yake. Nimeliangalia hili neno, nalifahamu lakini sikulipata vizuri, ni huruma au sijui ni nini, nikasoma kwenye Kamusi maana yake ni kukirimu wageni, shilingi milioni 300 kasoro milioni moja yaani milioni 299. Idara ya Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao ina shilingi milioni 63. Mimi nimeomba shilingi milioni 40 tu ili nipeleke watu wangu wa Bukoba waende wakajifunze namna ya kupambana na mnyauko, lakini sijapewa, wanabajeti shilingi milioni 300 kukirimu wageni, hii sikubali. Tupo hapa kwenye bajeti, si ajabu Maafisa wote wa Kilimo wapo Dodoma wamekuja na kila mtu na gari lake, wasikae wanne kwenye gari kwa nini halafu wakaja hapa? Kwa hiyo, hii kwa kweli hatutaelewana. Kama nilivyosema nitasubiri Wizara ya Kilimo ifike tushikane mashati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda haraka na mengine nitayaruka, lakini la mwisho ni kuhusu kilimo pia. Tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo na ni kweli kwa sababu bado uchumi wetu unategemea sana kilimo. Lakini hatufanyi vya kutosha kwenye jambo hili, tuna ardhi nzuri sana Tanzania, ukitembea nchi hii utaona mabonde mazuri kila mahali kwa mfano Kilosa, Mvomero, Sumbawanga, Kigoma na kadhalika. Tuna vijana wengi wengi wamekaa mijini hawana ajira, mtu anauza barafu, pipi, peremende au kandambili moja, fanyeni utaratibu mzuri, panga maeneo haya ya ardhi kisha peleka vijana kama 500 iwe kama kambi.

Mheshimiwa Spika, tuna mpango wa Kilimo Kwanza, wapelekeni kule lakini msiwatupe kama Manamba. Tuwapeleke lakini tuwape pembejeo kama matrekta, *powertiller*, pembejeo, madawa, mbolea na kadhalika ili waanze kulima kwa mkopo siyo bure na wapate na huduma kama ni mabati au maturubai wajenge nyumba za haraka haraka, wapate Waganga wa kuwasaidia wakiugua Malaria hizi za haraka haraka, ulinzi na mgambo wenye silaha ili wafanye kazi ya kilimo na ni kwa matrekta siyo kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya miezi mitatu kama ni mahindi ni miezi mitatu na kama ni maharage ni miezi miwili, kama ni alizeti na kadhalika tutapata mafanikio makubwa kwa kupata mazao mengi sana ndani ya muda mfupi. Watu hawa baada ya muda mfupi kwa sababu tumewafadhili, tutapata mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa nimwite Mheshimiwa Aliko Kibona, atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika mjadala wa Bajeti iliyo mbele yetu siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia labda nianze na jambo moja ambalo asubuhi ya leo wakati wa maswali kwa Waziri Mkuu limenigusa na naamini kila Mbunge ameguswa, ni swali lililoulizwa na

Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, suala zito na nyeti linalohusiana na dalili za mgomo wa Madaktari.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wenzangu ambao nahisi hawatapata nafasi ya kuzungumza kwa sababu ya wakati ama hawatapata nafasi ya kuzungumza kwa sababu ama wameshazungumza ama muda wetu hautatosha lakini nadhani na nahisi kila mmoja alikuwa anahitaji kuzungumza juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo kuhusu Madaktari tangu wakati ule wa mgomo wa awali ni kwamba Serikali imechukua hatua za makusudi kwa kiwango kikubwa. La kwanza Serikali imekubali kuwalipa Madaktari *on call allowance.* Taarifa nilizonazo pia Ndugu zetu wataalam wetu Madaktari waliomba kitu kinaitwa *post-mortem allowance*. Serikali imekubali kutoka shilingi 10,000/= na sasa itawalipa shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali pia imekubali kutoa chanjo kwa Madaktari, Bima ya *Green Card* Serikali imekubali. Mabadiliko ya uongozi, Serikali imefanya jambo kubwa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote mnaonisikiliza, Serikali imemwondoa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Daktari Mkuu, Waziri wa Afya na imemwondoa pia Naibu Waziri, ni mabadiliko makubwa na ni heshima kubwa ambayo nahisi Serikali kwa kweli imeonesha dalili ya kuwakubali wataalam wetu. Natoa rai kwa wenzangu na ndugu zangu wataalam Madaktari kwa sababu tayari tumekuwa na Waziri mgeni na Naibu wake

mgeni katika Wizara ile pengine nitashawishika sana kuona kwamba Madaktari hawasikilizwi, iwapo watampa nafasi huyu Waziri azungumze nao na wao wasielewane naye. Kwa hiyo, kwa kweli nawaomba tafadhali ndugu zangu Madaktari wataalam wetu mpeni nafasi Waziri wa Afya ili aweze kusikiliza kilio chenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, narejea kwenye bajeti. Walioiandaa bajeti hii ni wanadamu kama sisi, mchakato wa kuandaa bajeti unaanzia tangu Wilayani, unakuja Mkoani mpaka Wizarani na Wizara zote na hatimaye ku-*consolidate* mambo yote mpaka kwenye Kitengo cha Bajeti, Wizara ya Fedha. Nadhani tukisema kwamba bajeti hii haifai kwa asilimia mia moja tutakuwa tunawabeza vijana wetu, wataalam wetu waliopo Wizara ya Fedha, Kitengo cha Bajeti.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuandaa bajeti ni wakati mgumu kwani watu wanaacha familia zao kwa muda mrefu wakihangaika kwa ajili ya kuandaa makabrasha hayo. Labda tu kwa sehemu niwapongeze wale wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kuifikisha bajeti hapa ilipofika. Utekelezaji kama walivyosema wenzangu waliotangulia ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa mambo ambayo nadhani kwamba ni muhimu niyazungumze ili Mawaziri wanaohusika, Serikali na wananchi wangu kwa kweli kule Ileje, Mkoa wa Mbeya na Watanzania kwa ujumla waweze kusikia japo kwa muhtasari. Mwaka 2009/2010 Serikali ilifanya kazi nzuri sana katika

maeneo yote. Mwaka 2010/2011 kwa asilimia kubwa mambo yote yamedorora kwani Serikali haikufanya vizuri. Vipo visingizio vingi na vingine vinawezekana ni vya kweli kwamba kulikuwa na ukame na kwamba hakukuwa na umeme, kwa hiyo uzalishaji na kila kitu vilikwenda visivyo.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vichache ambavyo havikwenda sawa.  Kwa mfano, kilimo na mifugo tulifeli, uvuvi tulifeli, ujenzi tulifeli, viwanda tulifeli, uzalishaji tulifeli, sakata la umeme tulifeli na sekta ndogo ya ujenzi tulifeli. Nilidhani kwamba mwaka huu bajeti hii ikipita wenzetu Serikalini mjipange vizuri ili *report* hii itakaposomwa na Mheshimiwa Waziri wa Sera, Mheshimiwa Wassira tuweze kukuta mabadiliko na tuweze kupongeza kwani hapa hakuna cha kupongeza kwa sababu kila kitu kilikwenda vibaya.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha anasoma bajeti yake alisema kifu fulani tumefuta kodi, tulishangilia na kupiga makofi. Nilifikiri kadri atakavyoendelea atasema Wenyeviti wa Vijiji watalipwa posho, hakuna kwenye bajeti. Nilifikiri atasema Madiwani wataongezewa posho lakini sijaona kwenye bajeti, nilifikiri wazee watapata *pension* lakini sijaona kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, nimesikia watu wanalia juu ya kodi ya bodaboda, tumerukia sana vitu kusema hiki kifutwe, hivi utafiti umefanyika? Wapo akinamama wanaingia sokoni kila siku wanachajiwa shilingi 200 kuuza mchicha, je hao tumewafikiriaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda unakwenda na sasa niende Mbeya. Naomba Waziri wa Fedha na Mawaziri wanaohusika waje na bajeti nzuri kwenye maeneo yafuatayo:-

Barabara yetu ya kutoka Mbeya kwenda Chunya imesimama, naomba tusikie kauli kwa Waziri wa Ujenzi atakaposoma kwenye bajeti yake. Barabara ya Mpemba nataka kusikia kauli, lakini barabara ya kutoka Katumba kwenda Ruangwa, Tukuyu pia nataka kusikia kauli na zipo barabara nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Kiwira. Suala hili tulilizungumza kipindi cha Bunge lililopita kwamba linatuletea ugomvi. Nashukuru Serikali sasa inasema imepanga shilingi bilioni 40 kwa ajili ya kulipa madeni na vitu vingine, nataka wakati Waziri wa Nishati na Madini akileta bajeti yake anifafanulie na wananchi wa Ileje, Mbeya, Rungwe, Mkoa mzima wa Mbeya wasikie kazi itaanza Kiwira.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikia mazungumzo ya habari kuhusu uanzishwaji wa Halmashauri mbalimbali katika nchi yetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, ni kengele ya pili!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na sasa nitamwita Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Abia Nyabakari ajiandae na Mheshimiwa Freeman Mbowe pia ajiandae.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii muhimu ambayo ni mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Kabla sijaanza kuchangia napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wale Mawaziri waliochaguliwa baada ya mabadiliko ndani ya Baraza la Mawaziri. Wote nawatakiwa mema kwa kazi walizopewa. Pia ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wabunge tuliowachagua kutuwakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki. Ningependa kuwataja majina yao kama ifutavyo: Shyrose Bhanji, Abdullah Mwinyi, Charles Makongoro, Twaha Issa Taslima, Nderakilo Kessy, Bernard Musomi Murunya, Angela Charles Kiziga, na Maryam Ussi Yahya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya kazi nzuri tuliyoifanya hapa nadhani na wao watatuwakilisha vizuri. Nawatakia kazi njema huko ingawa najua bado wana kesi ambayo inawakabili, nadhani wataimaliza mapema waanze kazi zao. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu safari hii ni mdogo sana, siyo mkubwa. Ningependa kuelekeza kazi yote kwenye mambo makubwa mawili: Moja, bajeti hii inaonesha kwamba mapato yote ya nchi

kiujumla ni kama trilioni 15 na kati ya hizo ni trilioni nane (8) tu ambazo ndiyo sehemu ya mapato yetu ya Serikali. Katika fungu hili utaona huyo ndiye Sungura ambaye tunataka tumgawane, hizo fedha chache. Sungura huyo ni mdogo sana kama wanavyosema, ni asilimia 30 tu itakayokwenda kwenye maendeleo nchi nzima. Kwa hiyo, mapato yetu kutokana na *speech* ya Waziri ni kwamba ni madogo sana. Kwa nini ni madogo nchi ambayo imejaa migodi mikubwa? Wanaofaidi ni akina nani? Mimi sijui!

Mheshimiwa Spika, ukichukua kwa mfano, mgodi wa Buhemba uko pale miaka na miaka lakini unaliwa na watu. Hizo fedha haziendi kuhudumia ama kusaidia wanyonge wa Mkoa wa Mara au Buhemba tu yenyewe. Ukiongeza na Kiwira ambayo nitaizungumzia baadaye kwamba, hii migodi miwili tu ingeweza kufuta idadi ya fedha ambazo Serikali inapata kutoka kwa wafadhili. *(Makofi)*

Sasa mnaposema fedha hakuna, mimi sielewi. Watu wangu wa Mara hawana fedha. Barabara zao hazipitiki. Jimboni kwangu shule hakuna. Lakini ukiangalia kwenye bajeti hii nasikia bilioni 40 zinakwenda Kiwira kuwalipa wale ambao wamenunua na wanasema kwamba wametumia fedha kwa shughuli zao wenyewe, lakini tunalipa bilioni 40 kama kulipa madeni yao. Ni madeni yapi hayo? Hizo bilioni 40 zingeweza kujenga chuo cha Mwalimu Nyerere tunachotaka kujenga pale. Chuo Kikuu kingejengwa kwa bilioni 40 hizo tu. Lakini zinakwenda kulipwa kwa watu ambao nataka kuwataja hapa. Tunakwenda wapi basi?

Mheshimiwa Spika, pale Buhemba naona kwenye bajeti wamesema wametenga bilioni moja yaani vijisenti kwenda kufufua Buhemba. Sasa unajiuliza Buhemba hii aliyeichakachua ni nani, ni Serikali ama ni nani? Serikali ndiyo imechakachua pale Buhemba. Kila kitu kimeporwa pale, lakini hapa tunasema kasungura kadogo sana kamebaki, hakuna fedha za maendeleo. Sasa tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fedha zingine mlizosema bilioni 40 kwenda kulipa watu fulani pale Kiwira. Lakini Kiwira ina sehemu mbili; moja ni Koburu ambayo imeuzwa kwa Waaustralia. Nitaomba uniruhusu nisome wanaojua nani yuko Kiwira, kwa nini tena tunalipa bilioni 40 na kwa kazi gani aliyoifanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitasoma yaliyotokea tangu mwaka 2007. Mwaka 2007 Bunge hili hili tuliamua kwamba, *Tan-power Limited* irudishwe kwa Serikali. Mwaka 2011 inaonekana kwamba, *Tan- Power* iliuzwa kwa Waaustralia. Lakini *Tan- Power* ilipouzwa kwa Serikali naambiwa ilifanya ubia na watu wa *NDC*, iliuzwa kiasi gani? Kuna sehemu hizi mbili; sehemu moja ni Kiwira yenyewe ambayo ni kapu ambalo liko tupu lakini Koburu ndiye yenye mali na imeuzwa kwa dola laki saba (US$ 700,000) tu. Lakini thamani ya Koburu yenyewe ni trilioni za fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nani sasa anamiliki Koburu? Nikiangalia kwenye tangazo lao lililotokea kwenye mtandao linaeleza kuna kampuni nne (4): Moja ni *Intra energy corporations Limited*. Kampuni nyingine inaitwa

*NU Corporation Limited* ya Australia. Kampuni ya tatu ni *Intra Corporation Limited* nyingine. Yote haya ni makampuni ya watu wa nje waliokuja hapa nchini, Serikali ikawaruhusu wachukue hiyo biashara nzima ya Kiwira, Watanzania wenyewe hawana hata fedha.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni lini Bunge ambalo linaweza kuunda pengine kikamati kwenda kuangalia hali halisi ya Kiwira. Kulikoni Kiwira! Kama ikiwezekana kweli tunaona Kiwira lazima tuitaifishe iwe mali yetu tena na Koburu irudi. Ikirudi hizo fedha zinaweza kugharamia kazi ambazo tutazitaja hapa nchini. Sioni kwa nini Serikali inaanza kukwepa kwepa tatizo la Kiwira. Ningependa nijue hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hilo nazungumza sasa mambo ya pamba katika Mkoa wa Mara. Pamba ni zao kubwa kweli ambalo zamani hizo Watanzania wengi sana walikuwa wanatumia fedha zake kufanya mambo yao yote wanayohitaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante!

**MHE. NIMROD N. MKONO:** Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, lakini naomba Serikali iichunguze Kiwira. (*Makofi*)

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kusema hivi, tafuteni kuwa na amani na watu wote. Tafuteni kuwa na utakatifu huo

kwa kuwa hakuna atakayemuona Mungu asipokuwa na huo utakatifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali au Wizara ya Fedha imetenga shilingi trilioni 10 kwa ajili ya matumizi na huo ndiyo ukweli. Napenda niwaambie wananchi wangu wa Rukwa kwamba, kwanza fedha hiyo imetengwa kwa sababu gani: Moja ni kuendesha nchi. Mbili, ni kuhakikisha nchi inatawalika. Tatu, kuviimarisha vitu vilivyokuwepo ili viendelee kuwa katika hali safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huwezi kutawala nchi kwa kupiga porojo na maneno, wafanyakazi hawatakuelewa. Shule zetu zinahitaji kukarabatiwa, Wanajeshi wanahitaji mishahara, maana wasipopata mishahara watapindua nchi. Barabara hizi tunazotembelea zinatakiwa kufanyiwa ukarabati, Manesi, Polisi wasipopewa mishahara hawatafanya kazi na nchi haitatawalika. Kwa hiyo, lazima Serikali iweke bajeti ya matumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitakapokuwa nikiunga mkono hoja hii wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Watanzania kwa ujumla watuelewe. Leo Mheshimiwa Mbowe amesema tena kuna mgomo wa Madaktari unakaribia kujitokeza tena. Ngojeni niwaambie, kitu kitakachosababisha tabu duniani ni pamoja na migomo na maandamano ya wafanyakazi na watu wanaokaa mijini bila kufanya kazi. Kuna kitabu kinaitwa *last events* kimesema juu ya mambo hayo. (*Makofi*)

Ndugu zangu Manesi na Madaktari, sisi wote ni wamoja katika nchi hii, tukae chini tuangalie. Kuna vitabu vimeandika maarifa yataongezeka na ajira zitakoma. Sasa ikiwa ajira zitakoma, tutaandamana kwenda wapi? Maarifa yameongezeka. Leo tunaona huendi benki tena kuuliza salio, huendi tena Ulaya kuuliza gari na wala leo huchanganyi tena kokoto kwa sababu kuna vitu vinachanganya. Kweli ajira hazitakoma? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Zitakoma, tujiajiri!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, Waganga juzi waliandamana. Kweli tunafahamu kwamba ni sekta nyeti, wakaleta madai yao kumi (10) sisi sote ni mashahidi. Serikali ikasema jamani sisi tunaweza kujikuna tunapofikia. Wakasema *on call allowance* tutatoa. Tena wakaongeza wakasema kwa wale wanaofanya *post-mortem* tutatoa *post-mortem allowance* kutoka 10,000 mpaka 100,000. Hiyo ni Serikali inafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu kuna *vaccination* ya *hepatitis,* wakasema nazo tutatoa. Wakafanya mabadiliko ya viongozi, kuna bima ya *green card.* Jamani Watanzania Waganga kuweni na huruma. Kazi itakayobaki duniani ni kazi ya Udaktari na Uganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani lazima ziweke bajeti ya matumizi ya Serikali. Sisi Watanzania hatuwezi kukwepa mikopo na misaada. Mtoto wa Mbuzi kamba ni yake. Bado hatujakuwa kiasi hicho. Hata Marekani

jamani inadaiwa zaidi ya trilioni 15.4 na kwa siku inachukua dola za Marekani 3.98. kila mmarekani anadaiwa zaidi ya milioni 80. Nashangaa watu wanasema Mtanzania anadaiwa laki nne na kitu, ni lazima tudaiwe jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusema ni rahisi lakini kutawala nchi siyo rahisi. Namnukuu Mheshimiwa Lowasa alisema: "Kuwa mtawala inatakiwa kuwa na maamuzi mazito wakati mwingine." Huo ndiyo ukweli. Lazima tukubali kwamba mikopo itakuwepo. Wachumi duniani wamesema anguko la uchumi lililotokea Marekani litazidhoofisha nchi zinazoendelea, zitakosa misaada ya ajira na hata Marekani yenyewe mwaka jana haikutoa huduma za kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ngoja nijielekeze kwangu maana naweza kusema mengi sana. Bajeti hii naiunga mkono kwa sababu imesema, miradi itakayopewa kipaumbele ni pamoja na barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi na sisi Sumbawanga ni namba moja, sasa ni muda wetu. Tumekuwa nyuma kimaendeleo kwa muda mrefu. Rais wetu, mkombozi wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete alituahidi barabara ya kutoka Gasensia – Matai. Kule kuna wafanyakazi inasemekana tangu mwaka 1961. Kuna Idara za Uhamiaji, Kilimo, Mifugo, Afya, Forodha na *TRA*. Hakuna hospitali, shule, wanalazimika kupeleka watoto zaidi ya kilomita tano(5). Pale mkituwekea barabara ya lami ndugu zangu tumepona, Wanarukwa tutapata ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji pia huu umeme unaotokea kuanzia huko Nyakanazi utakapopita Rukwa msisahau utaratibu wa kuweka Kiwanda cha Kutengeneza Chuma, Mkoa wa Rukwa. Milima yetu yote ni vyuma. Huo utakuwa ni ukombozi kwa Mwanarukwa na ndiyo maana nasema nitaunga hoja bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya Kiriamatundu–Mbeya–Kibaoni jamani zipewe kipaumbele kutuunganisha na sisi Watanzania. Tunahitaji Kirando iwekewe utaratibu kwa sababu pale ndipo tutakapokutana na Wazaire na pale Kasesya na Wazambia ili tubadilishane mawazo na sisi tuinuke kiuchumi. (*Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Safii.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Katika bajeti hii naomba Rukwa msiisahau. Sumbawanga Mjini, maji hakuna. Yaani tunakunywa maji machafu. Lazima mtujali la sivyo bajeti ijayo nitasimama hapa kuikataa bajeti yenu. Haiwezekani tunywe maji yenye uchafu na wakati tuna Serikali sikivu na mmesema maji salama na safi vijijini na mijini na sisi tuko mjini tunataka maji safi.

Mheshimiwa Spika, ushauri. Katika kuboresha Kilimo Kwanza hawa watu wanaoishi mjini bila kazi washughulikiwe na hasa wapewe wanajeshi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Basi.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwanza nilidhani mchungaji fulani anaanza tena hapa. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Freeman Mbowe, atafuatiwa na Mheshimiwa William Ngeleja.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mawazo katika mjadala huu wa bajeti ambao unaendelea mahali hapa.

Nampongeza sana Mheshimiwa Mgimwa na Manaibu wake wote na Mawaziri wote ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais. Nawatakia utumishi wa uvumilivu.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni na kama Mbunge, kuna jambo la msingi sana ambalo ningependa kulitoa kama ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa pande zote mbili. Kama ambavyo wengine wamezungumza ni vyema na ni lazima sana tuheshimiane ndani ya Bunge.

Huu ni ustaarabu wa maana tu ambao hauna tatizo lolote, ila pamoja na kustahimiliana ndani ya Bunge, kuna ulazima vilevile wa kuvumiliana katika kazi za siasa. Matusi hayajengi na dharau hazijengi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Meza yako iwe makini kutenda haki kwa pande zote mbili ukiwepo

wewe mwenyewe, Naibu wako, Wenyeviti wako kwa sababu haki itakapopatikana kwa pande zote mbili nina hakika mijadala ya Bunge itakuwa ya salama. Lakini pale Meza itakapoyumba na kutokutenda haki ya kutosha kwa pande zote mbili na kuonekana kwamba upande mmoja unaonekana una makosa na mwingine unabebwa ni jambo la kusikitisha sana na ninategemea kwamba litatunzwa ili tufanikishe kazi zetu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Waziri na timu yake wamefanya kazi kubwa sana, lakini kazi ambayo sisi wajibu wetu ni kuikosoa Serikali, ni wajibu wetu wa Kikatiba kabisa na ni haki yetu ya kimsingi kuikosa kazi ile na pale tunapotekeleza wajibu wetu huo tunasikitika sana kauli za kejeli, za matusi na hata za kuchukua bajeti ya Upinzani na kuichana na kuitupa na bado viongozi wa Serikali wanasimama wanampongeza aliyefanya kitendo hicho ambacho sio cha kistaarabu. Haya siyo mambo yanayojenga ustaarabu na heshima katika uongozi. Ni vyema kama viongozi na kama watu wazima wakiwemo Mawaziri tujue hata tunapopongeza tupongeze mambo ambayo yana busara kama tunakusudia kujenga Taifa letu.

Ni vyema wenzetu katika upande wa Serikali wakaelewa kwamba sisi kama Upinzani hatuna Makatibu Wakuu wa kutusaidia, hatuna Makamishna wa kutusaidia, tunajitegemea wenyewe kuweza kutekeleza bajeti hizi, wala hatutegemei fungu la Serikali kuweza kutekeleza bajeti hizi. Watu wanakesha maofisini wakifanya kazi, tunafanya *research* usiku na mchana tukategemea mheshimu mawazo yetu na

muelewe tunafanya hivi ili kuwasaidia ninyi muweze kutekeleza wajibu wenu kama inavyostahili kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, muda wa dakika 10 ni muda mfupi sana. Tunaweza tukabishana hapa sana tukatafuta sifa za kuongea sana kwa nguvu kwenye vipaza sauti, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba kuna makosa ya msingi tunayafanya kama Taifa. Sitakwenda kujadili kifungu chochote kwa sababu dakika 10 kwa kweli haziwezi kunitosha. Lakini la msingi sana ambalo ningependa kulisisitiza katika siku ya leo ni kama hatutabadilisha utaratibu wa Taifa letu wa kujitegemea, kama tutaendelea kuwa Taifa tegemezi kufikiria kwamba makampuni makubwa ya nje, kufikiria mataifa ya nchi za wenzetu yatakuja kutusaidia tuondokane na umaskini wetu, tunajidanganya. Haya yanakuja kuchuma na ni lazima yaje kwa sababu hatuwezi kuishi *in isolation,* lakini lazima tujipange kukabiliana na ushindani wa Kimataifa, ni lazima tujipange, kuona tunaweza vipi kutumia rasilimali tulizokuwa nazo, ni namna gani tunaweza kujitegemea kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu leo inakuwa dhaifu kwa sababu inashindwa kujitegemea, Serikali yetu inakuwa dhaifu leo kwa sababu inaomba sana, Serikali yetu leo inapoteza heshima katika jamii ya kitaifa na pengine kimataifa kwa sababu inashindwa kujitegemea. Sasa Serikali inaposhindwa kujitegemea, Taifa linaposhindwa kujitegemea hadhi ya Taifa ni lazima itashuka.

Mheshimiwa Spika, sasa nimesikia baadhi ya Wabunge hapa wanapongeza sana hoja ya kukopa. Ni kweli nchi mbalimbali zinakopa, lakini tunakopa kufanya nini na tunakopa kwa viwango gani? Tusisahau Waheshimiwa viongozi katika miaka michache iliyopita nchi yetu ilifarijika na Mpango wa *HIPC* wakati wa utawala wa Mheshimiwa Rais Mkapa, ilikuwa dhumuni ni kufuta deni la Taifa na Rais Mkapa alifanya kazi nzuri sana kwa kipindi kile, lakini leo tuko wapi baada ya mafanikio makubwa tuliyoyapata wakati wa *HIPC?*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mserereko wa bajeti ya Taifa kwa miaka 10 iliyopita, Waheshimiwa viongozi tuki-*compute* katika *dollar terms* mwaka 2001/2002, Bajeti ya Serikali ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa ni Shilingi trilioni 1.412 na ya maendeleo ilikuwa ni Shilingi bilioni 352. Ukiweka katika thamani ya Kimarekani mwaka 2001/2002 ambayo ni miaka 10 iliyopita, tulikuwa tuna bajeti ya Dola za Kimarekani Shilingi bilioni 2.2.

Mheshimiwa Spika, leo tuna bajeti ya Dola za Kimarekani Shilingi bilioni 9.5. Lakini ukiangalia matumizi makubwa yamekwenda katika miradi mbalimbali ambayo *actually* katika uendeshaji wa Serikali, tunapanua sana utawala wa Serikali, tunapanua Mikoa, tunapanua Wilaya ndiyo tunafanya kazi katika *infrastructures,* lakini vilevile tunapanua sana utawala wa Taifa hili na fedha nyingi ambazo zingeweza zikawasaidia wananchi wa kawaida, zinakwenda katika masuala ya kiutawala. Sasa kama mambo haya hatuwezi kukubaliana kama Taifa tukaona *priority* yetu

ni kupanua utawala ama kupanua huduma kwa wananchi, tutakuwa bado tunaendelea kulalamika na hakika majuto yatakuwa ni mjukuu.

Mheshimiwa Spika, siyo jambo jema kama Taifa ama kama viongozi kujisifu kuwa masikini. Mara nyingi zimetolewa *sentiment* za kuonyesha kwamba huu umasikini ndiyo sehemu ya heshima ya uongozi, siyo kweli. Mimi naungana sana na Mheshimiwa Cheyo katika sera yake ya utajirisho na mapesa hatuwezi kujenga Taifa la viongozi ambao unafikiri umasikini ni heshima, umasikini ni udhalimu, umasikini ni aibu. Ni lazima viongozi tutamani Taifa hili liwe tajiri, wananchi wawe tajiri na tuweke mikakati ya wananchi kuwa tajiri. Huo ndiyo ustaarabu na bila ya kuwa na hiyo *trust,* bila ya kuwa na hiyo *dream* tutaendelea kudanganyana hapa kwamba umaskini ni utajiri na kwa kweli inatuondoa katika msingi mzima ambao tunaukusudia kuusimamia kama viongozi.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja ya deni la Taifa kutoka Shilingi trilioni 10.5 kwenda 14 halafu tunajisifu kwamba tunakopa, tunakopesheka *and then we are proud of ourselves,* tunakwenda kukopa, angalieni katika mwaka huu wa fedha tunakwenda kukopa madeni ambayo ni mikopo ya masharti ya kibiashara ya ndani ni 10.78 ya bajeti, mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ni 8.25%, hizi ni karibu *20% of the budget* tunakwenda kukopa. Masharti ya kibiashara, mimi bahati nzuri ni mfanyabiashara, masharti ya kibiashara zile benki zinatafuta faida na hakuna mahali benki zinaona raha kufanya biashara, napo kama Serikali, kwa sababu hiyo ni imani, ni *guaranteed*

kwamba itarudi. Lakini *at the end of the day,* nani anabeba hii *burden* ya kuja kulipa hili deni?

Kama Mheshimiwa Mkapa aliweza kushusha deni la Taifa katika Serikali hii hii ya chama hiki hiki, leo Serikali hii hii inaona *proud* kukopa na kuongeza tu mikopo, halafu tunafanya mikopo kwa sababu ya *recurrent expenditure.* Mimi nafikiri katika maeneo mengine siyo sahihi. Waheshimiwa viongozi, tuone aibu kukopa, tuone aibu kuukumbatia umasikini, tuone kwamba tuna sababu ya kutafuta mikakati ya ndani. Tunaingia katika *treaties* mbalimbali za kibiashara na mataifa ya nje kwa sababu ya kuweza kuingia kwenye mifumo huru ya kibiashara. Lakini sisi tunawapa nini wenzetu *against what we receive,* ni lazima kuanza kufikiria upya kama *WTO* inatufaidisha nini? Tunaingia mikataba, tunafungua soko letu linakuwa huru kwa kila mtu. Tunalinda vipi viwanda vyetu vya ndani? Tuna *import* pini leo, tuna *import* vifungo ni kwa sababu hatulindi viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, sisi hatutaunga hoja mkono bajeti hii kama Upinzani kwa sababu tunaamini kwamba haiwalengi Watanzania wengi ambao ni maskini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Unajua wenzenu tunaokaa katika Kiti hiki tunafuata kanuni ya Nane, lakini uzuri wake ni kwamba kila mtu analaumu tu, hakuna Mwenyekiti aliyekaa hapa hajapata lawama. Tunazo tu moja moja, mwingine toka nimeingia hapa sijauliza suala la nyongeza na vitu kama hivyo. Kwa sababu ni kiongozi,

hapa tunayapokea yote, lakini ukweli tunatumia kanuni ya nane.

Tunaendelea na Mheshimiwa William Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ramo Makani.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuiona siku ya leo. Lakini niseme tu kwa dhati kabisa kwamba mwezi mmoja na nusu uliopita nilikuwa Waziri wa Nishati na Madini. Kwa namna yoyote ile na kwa hali iliyokuwepo na kwa fursa ambayo nilipewa kuwatumikia Watanzania ni jambo la kheri kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Watanzania, kwa heshima waliyonipa kwa kuwatumikia Watanzania katika Wizara ya Nishati na Madini kwa zaidi ya miaka mitano, nawashukuru sana. Bado niko imara, naendelea kuwatumikia Watanzania kupitia nafasi hii ya uwakilishi wa wananchi. Nawatumia salamu wananchi wa Jimbo la Sengerema na familia yangu kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiniunga mkono. Nawashukuru sana Wabunge kwa jinsi ambavyo mliniunga mkono na kuniimarisha kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kwanza kabisa kuishukuru sana Serikali kuleta bajeti ambayo

inajibu matarajio ya Watanzania, imejielekeza katika vipaumbele ambavyo tumekubaliana Watanzania bila kujali itikadi za vyama, lakini pia inazingatia ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi na inazingatia changamoto zilizokuwa sasa. Hivyo kwa vyovyote vile, sina sababu ya kusita kuiunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Bajeti ni mjadala kuhusu mapato na matumizi na kwa vyovyote vile, kwa sababu bajeti hii imejielekeza vizuri kwenye Mpango wa Miaka Mitano ya tuliyoasisi mwaka juzi ambao inatupeleka mpaka mwaka 2015/2016 na kwa sababu vipaumbele viko wazi pale, lakini pia imezingatia changamoto za wakati huu zikiwepo hatua zilizochukuliwa na Serikali, naomba Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu waiamini Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na waiunge mkono kwa juhudi zinazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba uchumi wa dunia umeyumba na sisi Tanzania ni sehemu ya dunia. Lakini Tanzania kama nchi, hatutakaa kimya. Serikali na Chama pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge tumekaa pamoja kujadili mambo ya kuiokoa nchi hii kuitoa hapo ilipo na kuisogeza mbele pamoja na changamoto zinazoikabili nchi. La kwanza, tumeambiwa hali ya maisha ambayo sasa hivi inalikabili Taifa, imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mambo mawili. La kwanza, ni hali ya upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo ya Tanzania. Hilo liko wazi na limesemwa. Lakini la pili, ni kutokana na bei za gharama za bidhaa kama mafuta pamoja na masuala ya umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeambiwa hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali. Kwa kipindi kile kwenye upande wa chakula, Serikali iliruhusu kuagiza sukari pamoja na kusambaza vyakula katika maeneo ambayo yalikuwa yana upungufu. Lakini lingine kubwa ambalo Serikali ililifanya kwa upande wa nishati ni kuruhusu utaratibu wa kuendelea kupanga bei elekezi na kikomo kwenye mafuta uendelee, na kwa utaratibu huo uliosimamia *EWURA* Watanzania tunavyoongea leo kuna unafuu angalau wa asilimia ya 30 kuliko gharama ambavyo zingekuwa kama sio utaratibu huo. Lakini mpango wa kudhibiti mgao wa umeme tuliupitisha hapa Bungeni mwaka jana, 2011 Agosti na huo ndiyo ulitusaidia kutupa afueni ambayo tunayo sasa ya huduma ya nishati ya umeme. Vinginevyo, hali ingekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, wako watu wanasema eti hata kama juhudi hizo zimechukuliwa, haijaonyesha matokeo mazuri kuliko ambavyo ingekuwa. Lakini tunasema, bila juhudi zetu tungekuwa wapi? Serikali imesema ili kuendelea mbele zipo hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa. Tumeambiwa Serikali inakuja na utaratibu wa kuwekeza katika mabonde makubwa ambayo yako ndani ya nchi yetu yanayowezesha uzalishaji mkubwa wa chakula. Hili ni jambo la wazi ambalo litatutoa nchi hii kwenda upande wa pili. Lakini Serikali imesema itapitia vivutio pia na hasa kuhusu rasilimali iliyoko ndani ya nchi yetu na hasa viwanda ambavyo viko hapa vinavyotegemea malighafi za ndani ya nchi, itapitia vivutio hivyo ili kujenga mazingira ya kuviwezesha viwanda vya ndani

viendelee zaidi, vitoe ajira, lakini vipunguze mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa kuna suala la pamba na naomba ku-*declare interest* katika eneo hilo. Mimi ni mdau katika eneo la pamba. Wale Watanzania milioni 16 wanaosema kwamba wanategemea kilimo hiki, mimi ni mmojawapo. Tunaishukuru Serikali kwa sababu tuna taarifa kwamba inaendelea kupitia jambo hili kwa haraka sana ili kuhakikisha kwamba bei ya pamba inaimarishwa na kama alivyosema Mheshimiwa Mtemi Chenge, Sh. 1,000/= *book* hili lililosemwa, nadhani ni kwa kuanzia hapo. Mwendo huo tukienda nao, lakini pia tukarekebisha vivutio vingine kuhakikisha kwamba viwanda vya pamba vinafanya vizuri zaidi kuliko kutegemea fedha kutoka nje, itatusaidia sana. Sasa katika mazingira haya, ni vyema Serikali kukubali juhudi zilizofanywa.

Mheshimiwa Spika, niongelee deni la Taifa. Yamesemwa mengi sana kuhusu deni la Taifa. Lakini tafiti zote na taarifa za kitaalamu zimeonyesha kwamba deni hili linahimilika na sisi siyo peke yetu tunaokopa. Zipo nchi kubwa duniani ambazo zinakopa na uwiano wa pato la Taifa na deni tumeonyeshwa. Tumekumbushwa kwamba Kenya leo uwiano wa deni na mikopo ya nje na mikopo wanayokopwa na deni la Taifa ni asilimia 48.9. Tumeambiwa Marekani ni asilimia 102. Wajapan wana asilimia 229, Ujerumani 81.5 na *Italy* 120. Sasa ni lipi ambalo linashangaza leo uwiano huu wa asilimia 44 kwa pato la Taifa? Nadhani wakati

mwingine Waheshimiwa Wabunge tunakuwa hatuko wakweli na hasa upande wa pili wanapojaribu kuwatia hofu Watanzania kama vile sisi tunaongea peke yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi kuna Waheshimiwa Wabunge upande wa pili ambako tunatazamana hapa, mmojawapo alisimama ni mtani wangu kutoka Iringa, akaongelea kuhusu umakini wa utayarishaji wa bajeti, lakini Mheshimiwa mwingine juzi naye akatukumbusha akanukuu msemo wa zamani. Mara nyingi mzimu uko katika maelezo. Mheshimiwa Mbowe kama Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, nakuheshimu sana na uhusiano wako na mimi, hauna mashaka yoyote. Lakini nataka niseme jambo moja tunaongelea habari kubwa na Kambi ya Upinzani inasimama hapa kujionyesha kama Serikali tarajiwa, mbadala, sio kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, umeliweka vizuri sana. Mheshimiwa Mbowe nakuelewa umeleta hotuba ambayo umeisoma hapa na wewe unasema unaleta *elements* za kibinadamu, tunakuelewa vizuri sana. Lakini makosa yako wazi ambayo hayawezi kuvumilika na ni upotoshaji mkubwa kwa Watanzania na nitakupa mfano.

Mheshimiwa Mbowe ukienda kwenye hotuba yenu ukurasa wa 24 na 25 mmejichanganya na kuwapotosha sana Watanzania na ni bahati mbaya kwamba bajeti yenu imetangazwa mpaka sasa hivi katika magazeti mawili tu, gazeti la Mtanzania la tarehe 20 Juni, 2012 na gazeti la Raia Mwema la jana

tarehe 20 Juni, 2012. Mlitangaza kwanza katika gazeti la Mtanzania tarehe 18 Juni, 2012, na mkatangaza katika tangazo la Raia Mwema jana tarehe 20 Juni, 2012. Lakini Watanzania wengi kwa sababu mijadala tunayoisema hapa Watanzania wengi wanaitumia kujadili, mmewapotosha Watanzania kwa kiasi kikubwa sana na nitaomba kama nakosea, omba mwongozo wa Spika nisome vifungu hivi.

Mheshimiwa Spika, wakati wenzetu wanalalamika kwamba bajeti ya asilimia 40 imetengwa kwa Wizara ambazo tumezipa vipaumbele, ukurasa wa 25 wanalalamika kwamba tumezitengea fedha kidogo sana. Wanalalamika kwamba bajeti kubwa wamepewa Wizara nne, tano ambazo tumezipa vipaumbele. Lakini watu walewale, hotuba imetayarishwa na watu walewale wenye mawazo yale yale wakijadili bajeti ile ile wanapingana na mawazo kwa kusema bajeti ile tumetenga fedha kidogo sana, tutakuelewaje? Mnajiandaaje kuwaandaa Watanzania kwamba nyinyi mnaweza kuwa Serikali Mbadala? Lakini nenda ukurasa wa 34, vyanzo vya mapato. Hii ni *patent error, fundamental* hatuwezi kuirekebisha, hii tunafanyaje?

Mheshimiwa Tundu Lissu, kama Mnadhimu Mkuu wa Upande wa Upinzani, kama nakosea sema, inakuwaje katika ukurasa 34 hamwonyeshi vyanzo vya mapato ya kodi? *TRA*, mapato yasiyo ya kodi, mapato ya Halmashauzi, *zero*.

Mheshimiwa Spika, naomba nitahadharishe hapa; ni rahisi sana kupanga bajeti ya harusi ama bajeti ya

maandamano. Kupanga bajeti ya nchi ni jambo kubwa, linahitaji umahiri mkubwa. Tusiwapotoshe Watanzania, mnawanyima fursa ya kusema habari zenu kwa sababu hawana hii bajeti, imetangazwa katika magazeti, wale wangapi hawana *access.*

Nafahamu katika mjadala huu unaweza kuwa na agenda, wewe na wenzako ya kutoka nje ya Bunge hili. Kwa sababu mnaficha aibu, naomba muinue nyuso zenu, Watanzania wawaone kwenye televisheni jinsi mnavyoupotosha umma kwa kutowaambia ukweli. Kwa nini msingesimama hapa mkaomba radhi? Watanzania kule wanapasuana vichwa kwamba Kambi ya Upinzani imeweka Bajeti Mbadala. Bajeti Mbadala gani ambayo haina vyanzo? Mnawafanya Watanzania hawafikiri sawa sawa. Enzi hizo zimekwisha, lazima muwe wawazi. Sina hakika kama kwa Msajili wa Vyama kule hakuna habari ya kufuatilia kujua kama haya ninayosema sio ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana Watanzania na ndiyo maana utakuta mwisho wake kwenye hotuba hiyo Mheshimiwa Zitto anajinukuu mwenyewe, hivi nyinyi katika uongozi wenu, Mheshimiwa Mbowe ama Mheshimiwa mwingine, hakuna aliyewahi kutoa neno la busara akanukuliwa? Mheshimiwa Zitto anajinukuu tu hapa, yote hiyo ni kutuonyesha umakini katika maandalizi ya bajeti ambayo Watanzania watatarajia kwamba tunajadili mambo makubwa hapa, tunaongea mambo ya msingi na kutoa mwongozo ambao Watanzania kwa pamoja tunasaidia kujenga nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Watanzania wasiichambue bajeti hii

kwa kuiangalia kwamba tuna Bajeti Mbadala hapa, hakuna.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naendelea kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa msemaji aliyekwishakaa kwamba kinachojadiliwa katika Bunge hili Tukufu ni hoja ya Bajeti ya Serikali, moja. Pili, kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge hili Tukufu, hakuna kitu kinachoitwa Bajeti Mbadala ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika. naomba nimalizie. Tatu, kitu ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeleta Bungeni kinaitwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili, "Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Bajeti ya Serikali." Kwa haya maneno kwamba bajeti Mbadala haya ni maneno yaliyoko nje ya taratibu za Bunge hili. Bajeti inayojadiliwa ni Bajeti ya Serikali. Kilichotolewa na Kambi ya Upinzani ni maoni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nafikiri nijibu hili kwanza. Alichosema Mheshimiwa Tundu Lissu ni sahihi kwamba kinachojadiliwa ni Bajeti ya Serikali, hiki kinachoitwa Bajeti Mbadala, hakipo kwenye Kanuni na kwamba yaliyozungumzwa ni maoni. Hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, sasa maoni yale yanajadiliwa tena. Maana ukijadili maoni, niliwaambia jana Bunge linapaswa kufanya *dialogue*. Kwa hiyo, mnaweza kutoa maoni na wengine wakatoa maoni. Ndiyo inavyokuwa. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema tuendelee na mjadala.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Taarifa, Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nilisahau kukuuliza, taarifa unaikubali au huikubali?

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, taarifa naikataa, lakini wasome ukurasa wa pili. Kabla ya kutoa Bajeti Mbadala ya Kambi ya Upinzani, ni kitu gani hiki? *(Makofi)*

Msiwafanye Watanzania hawaelewi, hapa Watanzania wanafuatilia. Waombe radhi kama wanakana hiki kitab,u na hakuna haja ya kutupotezea nguvu hapa.

**SPIKA:** Nafikiri nimetoa uamuzi. Naomba tusikilizane.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Taarifa.

**SPIKA:** Naomba tusikilizane. Ndiyo maana kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Halima Mdee, naomba ukae kwanza, kiongozi wako alisimama sijampa nafasi. Ninachokisema ni kwamba, ni kweli suala la Bajeti Mbadala siyo Kanuni zetu. Kwa hiyo, limeendelea kwa miaka mingi, lakini siyo Kanuni zetu. Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, dhamira ya kusimama mahali hapa ni kuomba tu kutoa taarifa au niombe mwongozo wako badala ya

taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambacho kinasema: "*Hali kadhalika Mbunge anaweza simama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika*."

Mheshimiwa Spika, maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika ukurasa wa 35 ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuongea amei-*quote* kwa mbwembwe nyingi na makofi mengi imeonyesha *schedule* ambayo mapato ya ndani pamoja na mapato yasiyo ya kodi ambayo yote kwa ujumla yali-*amount to* trilioni 11,889,078,000/-. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Tulieni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Spika, sasa akijaribu kuwafahamisha Watanzania kwamba tumeleta maoni upande wa pili ambayo hayaonyeshi vyanzo vya mapato, siyo kweli. Sasa naomba mwongozo wako, wakati Wabunge wanapojaribu kupotosha kwa sababu tu wanapata fursa ya kuzungumza, Meza inayachukulia hatua gani? Kwa sababu hili jambo limeshatolewa mwongozo huko siku za awali. Bado wanali-*repeat* tena kwa nia ya kupotosha umma. Meza yako inatoa mwongozo gani?

**SPIKA:** Kwa sababu hili limekaa kitaarifa, naomba Mheshimiwa Ngeleja asome alichokisoma mwanzo.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaendelea kusema kwamba, namheshimu sana Mheshimiwa Mbowe, lakini ninachosema ni kwamba, tulifundishwa kule shuleni

mambo ya kweli hayabishaniwi. Nimenukuu ukurasa wa 34 ambao uko wazi. Sio wa 35 Mheshimiwa Mbowe, nafahamu kibinadamu hatuko timilifu, unaweza ukateleza. Ameteleza. Lakini ukurasa wa 34, sura ya Bajeti mbadala ya mwaka 2012/2013 iliyowasilishwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, upande wa mapato kushoto upande wa Shilingi milioni upande wa kulia. Mapato ya ndani (i) Mapato ya Kodi *TRA* 0/-. Ndiyo maana nikasema hii ni bajeti ya harusi. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Ambapo mnaweza kapanga Bwana harusi akaja akasema, sehemu ya koti ninayo inabaki sifuri. Mapato yasiyo ya kodi 0/-. Halafu (b) mapato ya Halmashauri 0/- lakini aggregate sum wanasema bilioni 11.8. Mheshimiwa Mbowe tunabishanaje katika mambo ya ukweli? Ndiyo maana nikasema waliosoma gazeti la Raia Mwema la jana na Mtanzania wataona Watanzania tunachokisema hapa ni cha ukweli bila kupotosha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilisema usome tu pale. Waheshimiwa hebu kaeni chini. Anapoongea mmoja anamaliza, halafu tunakuja na mwingine. Nilichosema, kwa sababu huyu anasema hesabu nyingine kumbe ukurasa tofauti na ule aliokuwa anasema. Kwa hiyo, naomba msome vitabu vyenu. Haya Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, natoa taarifa. Inaonekana Mheshimiwa Ngeleja ana uchungu wa kutemwa kwenye Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ondoa maneno hayo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hili suala...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mdee hebu ondoa maneno hayo! Kama taarifa ni hiyo, basi ukae chini. Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa yangu.

**SPIKA:** Kwanza uondoe yale maneno uliyosema kuhusu Ngeleja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hatuwezi kuruhusu...

**SPIKA:** Ondoa maneno uliyosema kuhusu Mheshimiwa Ngeleja. Naomba wengine wote mtulie.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwamba ana uchungu wa ku.... *okay*, nimefuta.

**SPIKA:** Umeyatoa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nimeyatoa hayo kwamba ana uchungu.

**SPIKA:** Basi endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nije kwenye kurekebisha hoja. Kwanza, inaonyesha ni namna gani hasikilizi na hahudhurii kwenye vikao. Kwa sababu hiyo hoja ilizungumzwa juzi na juzi hiyo hiyo Msemaji wa Kambi ya Upinzani alileta *amendment,* akaonyesha hii ilikuwa ni *typing error*. Akabainisha vyanzo vya mapato na ukitaka kuangalia, tafuta *record* ya *Hansard*.

Juzi Naibu Msemaji wa Kambi ya Upinzani – Mheshimiwa Christina Lissu, alileta na yakamalizika. Kwa hiyo, tusipoteze muda badala ya kujadili hoja za msingi, tunajadili mambo mepesi. Uchambuzi ulifanyika, wakitaka watafute *Hansard* ambazo ni *records* sahihi za Bunge zilizoonyesha mapato ya ndani kwa *TRA* kiasi gani, mapato yasiyo ya kodi kiasi gani? Mapato ya Halmashauri kiasi gani?

Kwa hiyo, kama Mbunge hana ajenda, anyamaze, asitumie Ukumbi wa Bunge kupoteza muda.

**SPIKA:** Haya, naomba tusiendelee kubishana hapa kitu ambacho hakina maana. Iwapo taarifa iliyoandikwa na wale wanao-*lay down on the table* hapa, kama kuna kasoro yoyote katika taarifa zile tunaleta kitu kinachoitwa *addendum*. Kwa taarifa zote zinazokuwa *laid down on the table* kwa taarifa zote mnazo-*lay down on the table* kabla ya kusoma kama kulikuwa na makosa yoyote yale, huwa zinaletwa *addendum*. *(Makofi)*

Naomba tuendelee na Mheshimiwa Eng. Ramo Makani atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na John Shibuda kama yupo.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye mjadala ulioko mbele yetu unaohusiana na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao.

Napenda kusisitiza kwamba, nitajikita kwenye mjadala wa Bajeti. Kwanza, nitasoma maneno ya utangulizi ambayo nimejiwekea kama mwongozo wakati nitakuwa najadili.

Mheshimiwa Spika, kwanza sisi kama nchi, tatizo letu kubwa siyo kutotenga fedha, hazitoshelezi kwa bajeti, bali ni kutotumia fedha tunazotenga katika kujenga uwezo zaidi wa kujitosheleza kibajeti.

La pili, tatizo letu sio kuwa na mipango mibovu na isiyotekelezeka kama baadhi yetu wanavyofikiri, bali ni kuwa na utekelezaji wa mipango kwa namna inayotuwezesha kubaini upungufu na kufanya marekebisho muafaka ili mipango hiyo ituwezeshe kufikia malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema hapo awali, tunajadili bajeti na mimi naomba wenzangu wakiwa wanajadili Bajeti hii wasiweke mbali sana nyaraka zifuatazo:-

Moja, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano tulioupitisha hivi juzi; Mbili, hotuba ya bajeti yenyewe, Bajeti ya Serikali. Lakini pia wakati wanatazama hotuba ya Bajeti wasiitizame yenyewe, ina *isolation*. Yenyewe ikiwa pekee, waangalie pia viambatanisho vya hotuba ikiwemo vile vitabu vine, kitabu Na. 1 mpaka Na. 4. Makosa mengi ambayo nimeyaona hapa ambayo yanatusumbua na tukijadilia, tunakuwa tunabishana sana, yanatokana na watu kusoma vitu nusu nusu. Sasa kwa sababu mimi napata nafasi ya kupitia, nataka niseme kwamba, Bajeti yetu ni Bajeti nzuri, ni Bajeti inayotekelezeka, ni Bajeti ambayo haijakiuka Mipango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ni Bajeti ambayo wala haijavunja Katiba kama wanavyosema wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo tumejiwekea vipaumbele. Vipengele vya kwenye Mpango wa Bajeti ni kama vifuatavyo:-

Ili kuokoa muda, nitasema tu vile vikubwa vikubwa badala ya kutaja vile vieneo vidogo vidogo vya chini. Miundombinu, huko ndani kuna vitu vingi vinavyoanisha miundombinu. Kwa mfano, Kilimo, viwanda, maji na huduma za majitaka. Lakini ya mwisho kabisa kwenye zile tano ambazo ukitaka unazikuta kwenye ukurasa wa 51 hadi 68 chini ya kichwa cha maneno *Core Priorities*, kuna nakala ile iliyoandikwa kwa Kiingereza. Sasa ile ya mwisho, ya tano inasomeka: "*Human capital development*."

Sasa kama *Human capital development* ni kipaumbele kwenye utekelezaji wa miaka mitano, basi

lazima tuulizane au tukumbushane hapa kwamba *human capital development* maana yake nini? Atakayeiondoa *training* kwenye *Human capital development* anashangaza kila mmoja.

Kwa hiyo basi, maana yake ni kwamba *item* za *training* zote kwenye kitabu namba moja, mpaka namba nne, zote zile kama zimewekwa mahali pengine nje ya kwenye eneo la Bajeti ya Maendeleo, natoa ushauri kwamba Waziri wetu wa Fedha apitie upya vipengele hivyo vya *training* hasa vinavyo-*support human capital development. Priority number five* ya Mpango wa Miaka Mitano vyote viende kwenye *development*.

Mheshimiwa Spika, sio *item* hiyo peke yake, nilisema watu wasome kikamilifu nyaraka zote zinazohusiana na bajeti. Kitabu namba mbili ambacho kwa bahati mbaya, siyo bahati mbaya, ndiyo utaratibu. Hivi ndiyo *public expenditure* kwa maana ya *services* ndiyo matumizi haya tunaita ya kawaida. Nimepita vipengele vingi sana, nikakuta kuna maeneo ambayo yakipitiwa upya baada ya kujadili na baada ya Waziri na timu yake kuyapitia, mtagundua fedha zimewekwa upande huu wakati zilitakiwa kwenda kule kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitasoma vichache tu hapa. Ukisema *new construction and other civil works,* kwanini hii iwe matumizi ya kawaida badala ya maendeleo? Muda haunitoshi, ningesoma tafsiri ya *development expenditure,* ipo. Lakini niseme tu kwamba *acquisition of cultivated assets,* hii *breeding stocks and live*

*animals,* hii inawezaje kuwa matumizi ya kawaida badala ya maendeleo? Unafanya *feasibility studies, project preparation and design,* halafu unasema matumizi ya kawaida siyo *development*. Naomba kwa ufupi tu Mheshimiwa Waziri ili kuwarahisishia wale ambao pengine wanaona uvivu kupitia nyaraka zote za Bajeti awasaidie tu kwa kutoa hizi *items* kutoa huku aende akawawekee kule wanakotaka zionekane moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo hoja zifuatazo zitajibiwa. Asilimia 35 tutaifikia au kuzidi. Mimi nilifanya hesabu kwa item chache sana tu hapa nikakuta tunakwenda mbali sana. Kwa hiyo, tutaondoka kwenye huo mtego na kwa hiyo, tutaondoka kwenye mtego wa kusema tumeweka fedha nyingi zaidi kwenye matumizi ya kawaida. Itakwenda ile maendeleo itapita hii nyingine iliyoko hapa. Mheshimiwa Waziri ajaribu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sasa nitoe mchango wangu kwenye *specifics*. Kwa kuwa muda unakuwa mfupi, niseme tu, tunapaswa ku-*address national agenda*. Mambo tunayojadili hapa na mengi sana yanayotupotezea muda, ukisoma Mpango wa Maendeleo, yote yapo na ndiyo yamewekwa kwenye *priorities*. Tumejipangia vizuri sana kwamba tukitekeleza hayo tutaondoka hapo. Hoja za kuwatumikia wananchi na kutekeleza mahitaji yao ya kiuchumi na kijamii ziko kwenye Mpango wa Maendeleo ambao wote tulishaupitisha hapa tayari. Kinachokosekana ni kuona namna gani tunatekeleza

na pengine tupate taarifa za mara kwa mara za utekelezaji wa yale ambayo yako kwenye Mpango.

Mheshimiwa Spika, nasema twende tujielekeze zaidi kwenye *national agenda* kwa sababu kila mmoja akisimama atasema maji, umeme, barabara, hakuna kipya. Yote yapo na kila mtu anafahamu. Sasa twende tujikite kwenye kutekeleza na ikiwezekana pengine Bunge hili liwe linapata taarifa za utekelezaji wa hayo. Unakuta hoja ilisemwa jana na mtu mwingine, kesho itasemwa na mtu mwingine, lakini ile ile. *National priorities* wote tunazifahamu, matatizo yetu yote tunayafahamu na yako *addressed* kwenye Mpango wa Maendeleo. Kwa hiyo, mimi ningetoa rai, Dkt. Mpango na Idara ya Mpango na Wizara inayohusika tuandalieni jedwali *detailed* za mambo yote yanayotakiwa kutekelezwa kutokana na Mpango wa Maendeleo, halafu mara kwa mara tuwe tunapitia kuona ni namna gani tunapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, *issue* ya migomo ya wafanyakazi, kwa kifupi sana nimesema twende kitaifa. Unajua ikinyanyuka *professional* hapa ikasema kwamba sisi ni muhimu zaidi tutekelezeeni zaidi; Madaktari wanagoma leo, kesho Walimu, Wahandisi sijui kwanini hawagomi, mimi nashangaa! Hoja hapa inatakiwa kwamba na nafikiri Serikali ilishapanga utaratibu, tulikuwa tuna Tume inafanya kazi ya kukusanya maoni na kuangalia namna gani tushughulikie suala la mishahara kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunashukuru umemaliza vizuri. Namwita Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Shibuda halafu Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka atafuata.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kushukuru, lakini niseme jambo moja haraka haraka. Mbele yetu tuna Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi wa Rais Mahusiano na Uratibu, tuna Hotuba ya Waziri wa Fedha. Hizi ndiyo zilizoko mbele yetu. Ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tujielekeze kujadili hizi, mengine ni mawazo na hata wenzetu wa Upinzani wametoa mawazo yao. Kwa hiyo, mimi sioni kama nina muda wa kuyajadili, maana ni mawazo tu. Nikianza kujadili mawazo ya kila Mbunge hapa nitapata shida. Cha msingi, nijadili Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo ulioletwa na Waziri, Mheshimiwa Wasira.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, naishukuru sana Kamati ya Fedha. Kamati ya Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Andrew Chenge amefanya kazi kubwa sana. Ukisoma hotuba ile ya Kamati ya Fedha unaona wametupeleka tujadili mambo mengi makubwa na ambayo tungeisaidia sana Serikali yetu. Cha kwanza, mfumuko wa bei ni tatizo kubwa. Serikali imetoa sababu na najua wanaendelea kuhangaika nalo. Lakini ningeomba sana watu wa Serikali watusaidie. Kwenye hili la mfumuko wa bei kuna *theory* nyingi sana. Lakini nadhani moja ya tatizo ambalo ni kubwa linalosababisha mfumuko wa bei na ambalo Serikali wameanza kulitekeleza ni suala la miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii tuna chumi mbili. Tuna uchumi wa mjini ambao una *inflation* na tuna uchumi wa vijijini ambao hauna mfumuko wa bei. Maana ukienda vijijini kwetu kule unakuta ndizi Sh. 500/=. Lakini ndizi hiyo hiyo ukiifikisha Dar es Salaam inakuwa Sh. 5,000/=. Sasa hizi Sh. 4,500/= ni nini? Lakini yule anayeuza ndizi Sh. 500/= akipelekewa khanga ananunua bei ambayo ina *inflation*; akipelekewa *cement* Dar es Salaam ni Sh. 14,000/=, Kigoma ni Sh. 22,000/=. Ukifikisha kule vijijini ni Sh. 25,000/=. Kwa hiyo, unaona, hapa tunazo chumi mbili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima tuzijibu kwa kufanya nini? Kitu cha kwanza tuwekeze sana na haraka kwenye reli, kwenye bandari, kwenye barabara, simu, kwenye viwanja vya ndege na kilimo cha umwagiliaji. Tumekisema sana. Umefika wakati sasa tuanze kutekeleza. Lakini pia tunazo barabara za vijijini. Ili barabara za vijijini ziweze kuleta mazao yao kwenye masoko ambayo watapata bei nzuri, ni lazima tuhangaike na masuala ya miundombinu. Naomba sana Serikali kwa juhudi ile ile mliyoianza na hili nalo tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni *export* ya ngozi ghafi. Ethiopia hakuna kusafirisha ngozi ghafi, Uganda hakuna kusafirisha ngozi ghafi, Botswana hakuna kusafirisha ngozi ghafi, kwanini sisi? Mimi nasema hii asilimia 90 ambayo Waziri amesema ya kodi, hapana, tu-*burn,* hakuna kusafirisha ngozi ghafi. Maana yake ni nini? Tutaongeza thamani kwenye ngozi hapa hapa

Tanzania, tutaongeza ajira na tutapata kodi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kodi za boda boda. Naomba sana zifutwe, vijana wetu mijini kote Tanzania wameamua kujitafutia ajira kwa njia ya boda boda, namna pekee ya kazi kubwa ya Serikali ya CCM ambayo mmekuwa mkiifanya, naomba tuwasaidie vijana hawa tufute kodi na kwa kufanya hivyo tutapunguza gharama za maisha yao.

Mheshimiwa Spika, suala la zero *rating* ya *textile industry*, tumeambiwa hapa kuna watu milioni 16 wakiwemo watu wa Kibondo. Kazi yao moja ni kulima pamba. Pamba hii bei yake tunategemea Soko la Dunia. Tukitegemea Soko la Dunia hatutawaendeleza wakulima wa pamba namna bora ya kuendeleza Soko la Dunia, lakini pia na viwanda vya ndani *(textile Industries)*. Siku zote kupanga ni kuchagua, Mwalimu alisema. Ninajua wapo watu, hasa watendaji wanasema hapa haiwezekani. Serikali ni yetu tufanye maamuzi. ondoeni hii kodi kwa ajili ya kuongeza ajira. Tukikuza viwanda vya ndani, bei ya pamba itapanda; lakini la pili tutatoa ajira na tutapata kodi. Hili Waziri wa Fedha ni suala lakufanya watu wasikubabaishe huko. Hapa ni suala la maamuzi tuyafanye.

Mheshimiwa Spika, suala la kodi ya *air time*, nashauri tuifute hii kodi. Wananchi Vijijini wanategemea simu hizi na maisha ni magumu, hatuwezi kuendelea kuifanya hiyo kazi. *Skill Development levy* wamesema ipungue kutoka asilimia sita kwenda asilimia nne, lakini watu wote tulipe *skill*

*development levy* kwa sababu sasa *skill development levy* inakwenda kusomesha watu mpaka Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, watu wote tuchangie, na ili watu wote tuchangie tuipunguze bei.

Mheshimiwa Spika, *VAT* kama tupo *under East African Community,* Kenya *VAT* ni asilimia 18, kwa nini sisi isiwe 16? Naomba tulitafakari. Lakini pia kuna suala la *annual motor vehicle license*, tunalipa *annual motor vehicle licence.* Mimi naomba leo nitoe ushauri wangu. *Motor vehicle license* ifutwe, lakini kwenye *road* tuongeze Shilingi tano, tukiongeza Shilingi tano maana yake nini? Tunafuta kodi ile ya *motor vehicle license*, tunafuta kodi ya boda boda, tumefuta kodi ya *air time*, hizi Shilingi tano zinakuja ku-*replace pale.* Naomba Waziri tulitafakari hili. Lakini pia suala la *VAT* kwa ajili ya wafanyakazi ama wafanyabiashara, *VAT* ni kila mwezi, *income tax* kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kupunguza gharama tuweke *returns* kwa miezi mitatu. Hili ni suala la kurasimisha biashara na iwe jambo jema.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni maji Kigoma, tafadhalini sana Mji wa Kigoma tuna maji mengi pale, lakini maji Kigoma hayatoki. La mwisho, naiomba Serikali na Wabunge tutafakari upya. Ninaliona lipo tatizo kubwa la mfumo wetu wa kibajeti.

Tatizo ninaloliona, tunaambiwa Shilingi trilioni tano kwa ajili ya maendeleo, Shilingi trilioni 10 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Lakini matumizi ya kawaida haya ukienda kuyaangalia sasa humo ndani kuna mishahara. Huwezi kuongoza nchi bila mishahara, lakini

humo ndani viko vitu ambavyo huwezi kuviepuka na mimi nasema hivyo vitu ni vya kimaendeleo.

Kwa mfano, Shilingi bilioni 440 ni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara ni kutengeneza barabara, mnawekaje kwenye matumizi ya kawaida? Lakini pia kuna Shilingi bilioni karibia 100 kwa ajili ya Bunge, ndani yake kuna kujenga Maofisi ya Bunge. Hii inakuwaje matumizi ya kawaida? Hapa pia kuna kujenga Mahakama, mmeiweka kwenye matumizi ya kawaida, tumeunda wenyewe Tume ya Kurekebisha Katiba. Tume hii gharama hii ni ya muhimu tunaweka kwenye matumizi ya kawaida, ununuzi wa chakula kwa ajili ya wananchi wetu kwenye ghala karibia Shilingi bilioni 39 tumeweka kwenye matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Shilingi bilioni 257 matumizi ya kawaida, kwa hiyo, ukiniambia mimi Waziri wa Fedha ninaona kuna zaidi ya Shilingi trilioni 2.3 ambazo mmeziingiza kwenye matumizi ya kawaida. Kwa kweli siyo sehemu ya matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, nasema hapa lipo tatizo la mfumo wetu wa kuandaa bajeti. Naomba wenzangu wa Wizara ya Fedha mtakapokuja, watalaam mtuambie, mchanganue vizuri ili tuweze kuwaambia wananchi. Ukipiga hesabu, ukisoma hivi vitabu, hela ya matumizi ya kawaida ni Shilingi trilioni 1.9 peke yake. Mengine ni matumizi ambayo *unless* mniambie tufunge Serikali, ni lazima yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema tupeleke ruzuku kwenye mahospitali; hivi kweli siyo wote tunataka

hospitali tupeleke ruzuku, sasa mnaitaje matumizi ya kawaida kwamba haya ni matumizi ya kula tu? Lakini tunasema ruzuku kwa ajili ya Mfuko wa Serikali za Mitaa, kila siku tunasema tupeleke maendeleo vijijini, kwenye Mitaa. Kwa hiyo, ninachoomba, watu wa Serikali mtusaidie sana. Naamini bajeti yetu ni nzuri na ninaona kuna *component* kubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kuwaambia, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati tuna Wizara tatu. Wizara ya Ujenzi, maendeleo peke yake ni Shilingi bilioni 693, *OC* ni Shilingi bilioni 329, lakini kwenye *OC* hapa kuna mishahara. Kwa hiyo, ukiondoa *OC* kwenye Wizara ya Ujenzi unakaribia Shilingi bilioni 800 kwa ajili ya maendeleo *against* Shilingi bilioni 200 kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ukienda Wizara ya Mawasiliano, Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, humo ndani kuna Shilingi bilioni 21 za mishahara, lakini kuna Shilingi bilioni 39 za maendeleo. Kwa hiyo, nasema *the way* tunavyopanga bajeti yetu hatuelezi hali halisi. Ninaamini Chama chetu kimefanya kazi kubwa kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono bajeti hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nimemwita Mheshimiwa John Shibuda, simwoni; Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Dkt. Limbu ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya nchi yetu kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, pamoja na muda mfupi, lakini nawiwa deni kuacha kukupongeza wewe, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu kwa njia ya haki na uwazi kabisa. Nina deni pia la kumpongeza Waziri wa Fedha – Mheshimiwa Dkt. Mgimwa na Manaibu Mawaziri wa Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa bajeti ya nchi yetu kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, na kwa wale waliopata nyadhifa mbalimbali, sasa uniruhusu nielekee kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu, na kwa kuwa muda wenyewe ni mfupi sana na mambo mengi ya msingi yamezungumzwa na pande zote mbili, Wabunge kutoka Chama Tawala, na Wabunge kutoka katika Kambi ya Upinzani, naomba na mimi niyakumbuke kwanza mambo ya msingi niliyotumwa Jimboni kabla sijakwenda kwenye masuala ya jumla ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kulieleza Bunge lako hivi leo, ni kwamba mtakumbuka mwaka 2010 tulipitisha Sheria mpya ya Madini, sheria ambayo iliwapa Watanzania kipaumbele, na kuhakikisha kwamba Watanzania watakuwa wanamiliki migodi ya madini ya vito kwa asilimia mia moja. Pale ambapo kuna haja ya

kumwalika, basi itafanyika hivyo kupitia Kamati ya Ushauri, itakayokuwa imeundwa na Waziri pamoja na Waziri mwenyewe kukubali kwamba ubia huo uwepo, lakini kwa namna ambayo haitamfanya Mtanzania kupoteza kuwa na nguvu katika umiliki wa migodi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Profesa Muhongo, ninamjua kwa muda jitihada alizokuwa akizifanya, nina imani kubwa kwamba ataendeleza kazi nzuri iliyokuwa imeachwa na Ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja na katika hili nakusudia kuzungumza leseni ya Kampuni ya *Tanzanite One* ambayo inatarajiwa kwisha wakati wowote kutoka sasa kama siyo mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mererani na wananchi wa Simanjiro na Watanzania kwa ujumla wao wanatarajia kauli ya Waziri wa Nishati na Madini juu ya mustakabali wa eneo lote la Kitalu 'C' inayomilikiwa sasa na Kampuni ya *Tanzanite One* iweze kuelezwa baada ya muda wao wa leseni kwisha. Ni matarajio yangu kwamba sheria iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu itazingatiwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu na sina mashaka na Waziri, sina mashaka na Naibu Waziri Masele, na hata mwenzake anayeshughulikia masuala ya nishati. Ni imani yangu kabisa kwamba Serikali itazingatia sheria hii kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, taabu kubwa tunayoipata katika migodi hii mikubwa na hili nalizungumza kwa uzoefu nilioupata kwa muda nikiwa katika Kamati ya

Nishati na Madini, lakini pia kwa uzoefu ambao wewe ulitupa fursa Kamati ya Nishati na Madini kutembelea katika nchi zinazochimba mafuta na gesi, na kwa maana hiyo tulipata nafasi ya kwenda Norway na baadaye nilikwenda mimi mwenyewe Sweden; kuna wenzetu walikwenda Trindad and Tobago kule wamepata uzoefu. Kule wenzetu wana utaratibu unaoitwa *Gas for Development, Oil for Development*, sisi huku ni lazima tufike mahali kwamba dhana hii ya wenzetu ambao wanatumia gesi na mafuta kwa maendeleo ya nchi yao, na hasa kwa Serikali kumiliki hisa kubwa zaidi katika migodi mikubwa, ni lazima Tanzania sasa ijielekeze kuwekeza katika migodi mikubwa ya dhahabu, ya gesi na hata katika uchimbaji wa madini mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na hisa kubwa badala ya kukaa na kutegemea *royalty* ambayo inatolewa baada ya mahesabu ambayo mara nyingi yanachakachuliwa kwa maslahi ya wawekezaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami ningependa kusema *gold for development, natural resources for development* na *development* ninayoizungumza ni ya Watanzania katika ngazi ya mtu mmoja mmoja na katika ngazi ya Watanzania kwa ujumla wao. Rai yangu kwa Serikali ya Chama changu ni kuelekeza nguvu kubwa kukusanya kodi kwa wawekezaji hawa. Tufike mahali tutangaze mgogoro na baadhi ya migodi mikubwa ambayo hivi sasa inahamisha uchumi wa nchi na wakati huo Tanzania inaachwa tupu na sisi wenyewe tunabaki kutegemea asilimia tatu ya *royalty* ambayo wakati mwingine Waziri ni shahidi, hata kwa muda mfupi aliokaa kwamba baadhi ya makampuni

yana mgogoro wa ku- *under declare* kile ambacho wanazalisha kwa maslahi yao. Tuondokane na fedheha hii. Kwa hiyo, natarajia kwamba Waziri ataweza kuweka hili bayana wakati wa bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimetumwa na wananchi wangu ni mgogoro uliopo kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Tarangire kwa upande wa Wilaya ya Simanjiro, na mgogoro uliopo kati ya Mkungunero *Game Reserve* na vijiji vya Kimotoro katika Wilaya ya Simanjiro, vijiji vya Rikyushibori na katikati katika Wilaya ya Kiteto. Gazeti la Serikali lililotangaza kuundwa kwa Mkungunero *Game Reserve* ilibainisha bayana kwamba Mkungunero *Game Reserve* itakuwa katika Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma, wakati nilipotoa rai yangu hapa na Mheshimiwa Nangoro akiwa Mbunge alipotoa hoja yake, ilipelekea Wizara kuelekeza Mikoa yote miwili, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara kuunda Kamati ya pamoja inayoweza kuangalia ukweli juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, wakati huo Mkoa wa Manyara ulikuwa unaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu na Mkoa wa Dodoma ulikuwa unaongozwa na Mheshimiwa William Lukuvi. Kamati zote mbili ambazo zilikaa pamoja na viongozi wa Mkoa wa Manyara zilibaini wazi kwamba Mkungunero *Game Reserve* imeingilia ardhi ya Wilaya ya Kiteto na ardhi ya Wilaya ya Simanjiro. Ni rai yangu kwamba nimetoka huko Jumamosi na Jumapili katika Kijiji cha Kimotoroku, Kitongoji chote cha Rakasupai kilichopo katika Kijiji cha

Kimotoroku chote kimemezwa na Mkungunero *Game Reserve.*

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, lipo eneo pekee linalounganisha Wilaya ya Simanjiro na maeneo mengine ya Mkoa wa Manyara ambayo hivi sasa Tarangire wana mpango wa kufunga na hivyo kupelekea kwamba eneo lile sasa Tarangire badala ya kuwa na kilomita za mraba 2,600 sasa linakuwa na kilomita za mraba 2,800.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwamba nitumie nafasi hii kukumbushia nafasi hii pia fidia ya mifugo katika Wilaya zetu za Longido, Monduli, Simanjiro, Kiteto na Ngorongoro ambayo Serikali iliahidi kutoa fidia. Hadi sasa imetoa mifugo 1500 badala ya kutoa mifugo 25,000 kama ilivyokuwa imeahidiwa katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Spika, narudi katika bajeti ya Waziri katika kifungu kile kilichokuwa kinatoa ahueni, naungana na wenzangu wa Kanda ya ziwa wanaozungumzia habari ya pamba na vivutio ambavyo vinapaswa kuwepo katika viwanda vyetu vya ndani na kuhakikisha kwamba ajira kwa Watanzania inapatikana. Ifike mahali hiyo, kodi muweze kuiondoa ili ushindani wa haki uweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo lingine kama wenzangu walivyozungumzia hilo, sina haja ya kuendelea sana. Ni rai yangu kwamba Waziri wa Fedha amelisikia na atahakikisha kwamba eneo hilo

nalo linashughulikiwa. Habari ya kuendeleza kutoza vinywaji baridi kama maji na soda, kodi inayoongezeka kila siku, tuelewe wazi kwamba Mikoa yetu ya Pwani na maeneo mengine ya nchi yetu bado maji yetu siyo salama kwa kunywa. Kwa hiyo, watoto wetu wanategemea kunywa maji haya ya Bakhresa, maji haya yanayotoka kwa wazalishaji wengine, na kwa maana hiyo, unapopandisha kodi maana yake unazidi kufanya maisha magumu ya Watanzania waliopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kuungana na wenzangu katika suala zima la kuhakikisha kwamba tunapanga bajeti ambayo inaitoa nchi yetu kutoka uchumi ulio nyuma na uchumi tegemezi na kuupeleka katika uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Ni rai yangu kwamba hatuwezi kufika huko kama hatuwezi kutoza kodi na kama hatusimamii matumizi ya fedha ipasavyo. Ugonjwa mkubwa unaoitafuna Serikali yetu kwa sasa ni ukosefu wa Watendaji waadilifu wanaiingiza nchi katika mikataba isiyokuwa na tija ambao wanatanguliza maslahi yao binafsi. Bahati mbaya sana haya yalikuwa katika awamu zilizopita, lakini sasa hivi naongeza kasi zaidi.

Tungependa kuona mikataba inayoingiwa sasa katika Sekta ya Madini na katika sekta mbalimbali inaweka mbele maslahi ya nchi badala ya kuweka mbele maslahi ya watu wachache wenye dhamana za umma katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu pia kwamba kwa kuwa maeneo mengi yamezungumzwa, nataka kugusia suala la kodi katika makampuni ya mitandao ya simu kama *Vodacom, Airtel* na wengine, kwamba sasa turudishe sheria ile ambayo imebadilishwa juzi juzi ili kuhakikisha kwamba wanajisajili katika Dar es Salaam *Stock Exchange*.

Mheshimiwa Spika, ni kengele ya pili au kwanza?

**SPIKA:** Ni kengele ya kwanza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru...

**WABUNGE FULANI:** Kengele ya Pili!

**SPIKA:** Ni kengele ya kwanza ya Pili?

**KATIBU MEZANI:** Ni ya pili!

**SPIKA:** Nasikia ni kengele ya pili, samahani sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza.

**SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Siwezi kubishana na Spika, naunga mkono hoja, ila masahihisho haya yaangaliwe huko mbele.

**SPIKA:** Unapoongea mazuri, saa inapita upesi. Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naona dakika zimekuwa chache sana, kwa hiyo, nitakwenda kwa haraka kipengele kwa kipengele kwa sababu mengi yamekwishasemwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri Mgimwa na Manaibu wake, Katibu Mkuu na Manaibu wake pamoja na Kamishna wa Bajeti - Mama Mamnyange na Ofisi yao nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwiwe radhi, kuna maneno nitakayozungumza ambayo pengine hayatafurahisha watu, lakini ndiyo ukweli na ndiyo imani yangu. Kwanza kabisa, kwa kipindi kama siku tano nilikuwa nje ya hapa Dodoma, nje ya Bunge kwa kazi nyingine, lakini nilikaa na wananchi wanaoangalia *Television.* Kwa kweli tafsiri zao na mwonekano unaoonekana ni jambo la ajabu, hadi kuna mmoja aliniuliza: Haa! Hivi kampeni safari hii zimeanza mapema! Nikamwambia hapana, ni Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa haraka, sasa hivi jamani hapa ndani ya Bajeti katika Bunge letu hili ni Tanzania kwanza, mambo ya Vyama baadaye. Tuna majukwaa ya kutosha huko nje ambayo tunaweza tukasema tukaelezea Vyama vyetu kwa wingi. Hapa ndani sasa hivi ni kuongelea maslahi ya

Watanzania. Sisi kazi yetu ni kusimamia Serikali na kuishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti, kwa pamoja tukae, kwa kweli inasikitisha, unashangaa watu wengine wana-*discuss* vitu tofauti kabisa. Mimi naomba niseme kwamba kwanza kabisa hakuna Bunge la Wapinzani, hakuna Bunge la Chama Tawala, Bunge ni moja. Ni lazima tuwe wamoja, tujadili mambo mamoja. Watu tunaowazungumzia ni wale wale, tuongee kwa maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimesema pengine mengine hayatawafurahisha sana, dunia nzima kazi ya Upinzani ndiyo hii wanayoifanya, hakuna jipya hapa. Kazi yao ni kupinga na wenyewe wanatamani kuingia madarakani. Kinachotakiwa, wanapopinga tatizo tu ni kwamba kuna baadhi yao sasa wanakwenda kinyume. Wana hoja, lakini hoja inafunikwa na lugha ambayo inaudhi. Kwa hiyo, pale ndiyo inakuwa tatizo. Lakini kazi ya Upinzani ni hii hii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wapinzani. Kwa nini nasema nawapongeza Wapinzani? Mtoto uliyemzaa mwenyewe anakwambia leo wewe mzazi baba au mama hapa umekosea hiki na hiki nia yake ni nini? Si urekebishe? Ufuatilie kama hakuna ukweli unaachana naye, kama ina ukweli, unarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wanatutakia mema, wanataka Chama Tawala tuendelee kuwa madarakani ndiyo maana wanatukosoa tujirekebishe,

ndiyo maana wanasema tuyafanyie kazi ili kesho na kesho kutwa tuendelee kuwepo. Mimi sioni kesi kabisa hapo. Kwa hiyo, naomba kabisa majukwaa ya siasa yawe nje. *(Makofi)*

Ndugu zangu inaonekana tunapoteza muda, hapa tuna siku tano tu hizi za kujadili hii bajeti, kesho tunapitisha bajeti hii, tumeiambia nini Serikali? Wako ambao kwa kweli wamezungumza hoja lakini walio wengi ni malumbano ya kisiasa, mimi naona kweli hii siyo nzuri. Hapa tushirikiane kwa pamoja, tushauri Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme lingine, Watanzania wa leo si Watanzania wa jana, wanaelewa. Hakuna Mtanzania nje asiyejua nchi hii imetoka wapi, imefika wapi na nani kaifikisha wapi. Mimi naomba niseme hivi, watu wanajua tunakwenda kwenye majukwaa tunaendelea kueleza lakini hapa ndani mimi nadhani watu wote wanajua, sisi twende kwa pamoja tuungane, hoja zimetoka Kambi ya Upinzani za msingi sana, hoja zimetoka Chama Tawala za msingi sana, haya ndio mambo Watanzania wanayotaka kuyaona. Jana nilikuwa na Askofu mmoja ananiambia sisi hatujali CHADEMA, hatujali CCM, hatujali nini tunachojali maslahi yetu. Sasa hapa tuko kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi. Kwa hiyo, niliona awali ya yote, niyasemee hayo kabla ya kuanza.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kuanza hoja zangu niseme tu na mimi nisipoteze muda kuongelea malumbano niende kwenye hoja. Kwanza kabisa, mimi kwa kweli nimeshukuru sana, wengi wameyasema

mambo ya msingi na kwa dakika 10 kwa kweli huwezi kusema mengi zaidi ya hapo, wengi wameeleza vizuri, wameainisha, ni imani yangu kwamba Serikali sasa itayatazama na kuyafanyia kazi kabla bajeti hii haijapitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza kilitumia mamilioni kama siyo mabilioni. Kimsingi mkiangalia hizi fedha zimewanufaisha wakulima wa kati kwenda juu, wakulima wa chini ni wachache sana. Nachukulia mfano wa Kilindi, Kilindi asilimia zaidi ya 80 ni kilimo lakini uliza walionufaika ni asilimia ngapi na maeneo mengine iko hivyo. Sasa leo hii unakuja unaona kilimo kinaachwa, sasa unajiuliza yale mabilioni na ile mikakati imekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, upande wa ufugaji, wafugaji ni wengi, tumesema tuache ufugaji kama huu ambao unafanyika kwangu labda wa kuhamahama na maeneo mengine, mikakati gani tuliyonayo? Chuo cha Utafiti Mpwapwa kimepewa shilingi milioni 700, hiki ni Chuo cha Utafiti, tunataka kusemaje, *are we serious of what we are saying?* Kwa hiyo, mimi nilitaka kusema hicho.

Mheshimiwa Spika, kingine, hawa Wachumi na Maafisa Mipango tunajiuliza wapo na kama wapo wanasikilizwa? Kwa sababu ukiuliza sana utaambiwa wapo wanatoa mawazo na hawasikilizwi. Mimi naomba hii Tume ya Mipango iongezewe nguvu ili tuweze kufanya vitu, utashangaa ndio maana maamuzi mengine unakaa unajiuliza, mimi mpaka leo hii najiuliza aliyeamua akatoa ushauri nyumba za

Serikali ziuzwe ni nani? Leo watu wanahangaika, wanatapatapa, Mikoa yote Viongozi wako hotelini, gharama kubwa, wengine wanatoka kilomita nyingi huko Dar es Salaam, mtu anatoka Kibaha anakwenda mpaka Mjini anaingia mpaka saa tatu na nusu, saa nne mnamtegemea afanye kazi na baadaye awahi foleni iliyoko huko. Sasa vitu kama hivyo ukiangalia unajiuliza kuna Wachumi na kama wapo kwa nini hawatusikilizi? Mimi naomba sasa tugeuzi, twende tuwape *priority,* tuwasikilize na tutekeleze ambayo wanasema kwa sababu kwa taarifa nilizonazo, wanazo hizo taarifa wanaweza wakatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *property tax.* Nilikuja na hoja binafsi kuhusu mapato ya Serikali, kwa bahati mbaya haikuweza kuzungumzwa lakini wamezungumza hapa lakini hii kodi ya majengo kwa kweli jamani nasema nitapata muda kwa sababu sasa nimeamua niifanye kwa njia tofauti ili muweze kuona, mchambue. Siyo siri, viongozi sisi wengi tuna majengo ambayo hatulipi kodi stahiki. Unakuta nyumba imekuwa *evaluated* tena kwa kukisia, *I think it is time now* kwa sababu tukipata kodi ya majengo peke yake kwa jinsi ambavyo ilichambuliwa na wataalam wale yaani inatosha kusaidia mambo mengi sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba nisemee hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pengine hamtaona la msingi ni jambo la UKIMWI. Sisi wengi hapa tuna UKIMWI, simaanishi ndani ya Bunge hili, ndani ya nchi hii.

**MBUNGE FULANI:** Hata hawahawa wanao.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Nasema ndani ya nchi hii lakini pia kuna watu tunaambiwa wafadhili wa UKIMWI wale wakubwa wanamaliza muda wao mwakani. Sasa mimi najiuliza, tuna mikakati gani maana hili jambo limekuwa *phased-out* na hawa ambao wanafaidika asilimia kubwa sana kwa dawa, vyakula na mambo mengi tunayoyajua, hawa hawafikiriwi mahali labda lipo mimi sijaliona lakini kwa kweli nimepitia sehemu nyingi sijaliona.

Mheshimiwa Spika, nikikaribia mwisho katika kulinda viwanda vyetu, jamani sisi Watanzania tumejitahidi kuwa na viwanda na tunaweza kuzalisha fedha lakini kama *VAT* kama wenzangu walivyoongea, mimi naomba kabisa hii *VAT* iweze kuondolewa. Vilevile tuangalie na kazi za wananchi wetu, wananchi huko mitaani wanalalamika sana vitu vingi, sasa matokeo yake wanavyolalamika inakuja hapa wakati mwingine labda tunapingana sisi wenyewe lakini jukumu lile ni letu sote CCM na hivi Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *Finance Bill.* Tunachukua muda mrefu sana kujadili matumizi, *what about* mapato. Najua labda wenzangu wamelisemea kwa sababu sikuwepo lakini suala la kujadili mapato kwa muda mfupi sana kwa kweli mimi naona hapa *we are not doing justice,* ili uweze kuzungumzia matumizi lazima uwe na mapato. Kwa hiyo, mimi naomba sana sasa hivi tubadilishe utaratibu, tupate muda wa kutosha kujadili mapato. Iko milango mingi ambayo haikuanishwa hapa, Mheshimiwa Waziri, sisi tuko na

wewe, tunajua uwezo wako, tumekuwa na wewe humu ndani Bungeni, tunaomba utusikilize Wabunge, pamoja na kwamba unasikiliza wataalam, tusikilize Wabunge, *we know more than what you should know from them,* kwa hiyo tutumie zaidi tuweze kukusaidia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niwapongeze sana vijana, kuna vijana wengi ambao ukiwasikia huko nje wanatoa tathmini ya mambo mbalimbali, nakumbuka siku moja nilikuwa nyumbani kwa Profesa Muhongo wakati bado yuko *South Africa,* walikuwepo vijana pale, walikuwa wanasema vitu ambayo unajiuliza hawa watu, *and they are not working, they are jobless.* Vijana wa *Clauds* wako pale, ukifungua radio kuanzia muda kama huu mpaka saa 12 jioni wana-*analyse* kila neno tulilosema, unakuta mtu anaipongeza bajeti nzuri lakini unashangaa, hapo anasema bajeti ni nzuri lakini ataichanachana vipande, tuwe waangalifu na tunayoyasema, tunaua imani yao, wanaona kama tunacheza mchezo wa kisanii. Kwa hiyo, mimi niwapongeze wale wote walioko nje ya Bunge hili ambao wanatusaidia kwa njia nyingine kuweza kuelimisha jamii kuona kwamba ni wapi tunatakiwa kwenda, ila pia watuletee na sisi taarifa tuweze kufanya yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, niombe tu kushukuru kwa haya yote, ni imani yangu kwamba yale tuliyoyasema hususani haya masuala ya kilimo na la *VAT* kwenye viwanda yatachukuliwa hatua ambazo tumeziomba zichukuliwe kwa sababu ni za msingi na ni muhimu sana. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kujadili bajeti ya mwaka huu wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Pili, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kazi kubwa unayoifanya. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi yetu. Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa na viongozi walioteuliwa na nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa sana aliyoifanya, pamoja na Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya mwaka 2012/2013, mimi mwenyewe nasema kuwa ni bajeti nzuri sana na inawajali Watanzania. Kwa nini nasema hivyo? Naongelea kuhusu vipaumbele ambavyo imeviweka mbele. Vipaumbele hivi, nikianza na miundombinu pamoja na umeme. Ili nchi iendelee, lazima iwe na umeme. Bajeti imelenga kuimarisha umeme wa mijini na vijini. Tufikirie kuwa tukipata umeme tutaimarisha viwanda vyetu. Umeme ukiwa vijijini hata vijana watakaa vijijini kwa sababu viwanda vidogovidogo vitaanzishwa. Umeme sasa hivi mimi niko hapa nashukuru kwa vijiji mbalimbali vya Mkoa wa Morogoro ambao ni wananchi walionituma hususan wanawake umeanza kuingia huko vijijini. Pia kwa Mkoa wa Iringa hasa huko Pawaga sasa hivi watapata umeme na tutaanza kukoboa mpunga kwa sababu tunalima sana huko mpunga. Tatu kwa kijiji changu Nyakayanga, Nyaishozi, Karagwe ninapozaliwa, hivi sasa tutapata

umeme, nashukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niongelee kuhusu kuimarisha reli ya kati ambayo inahusika na mambo ya usafirishaji na uchukuzi. Tunaposema kuwa hii bajeti haimjali Mtanzania, reli ya kati inamjali nani? Kama itaimarishwa, Mikoa yote inayotumia reli ya kati, Watanzania wote wanaokwenda huko kwa ajili ya usafirishaji na kusafiri, watanufaika. Kwa hiyo, inawajali Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumesema kuwa itafungua barabara ambazo zina fursa za uchumi. Barabara hizi zikitengenezwa biashara zitafanyika, usafiri utakuwepo na pia usafirishaji wa mazao utafanyika. Viwanja vya Ndege vikiwepo, tutapata wageni wengi na pia usafirishaji pamoja na masoko kila kitu kitafanyika kupitia kwenye mambo haya ya usafirishaji na uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeongelea kuhusu mawasiliano. Mawasiliano yakiwa mazuri, biashara zitafanyika kwa kutafuta masoko. Ila nilikuwa na ombi kwa Wizara zinazohusika, kwa vijiji vile na maeneo ambayo hawajapata mitambo, naomba sana waweze kupatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuongelea kuhusu maji safi na salama ambayo na yenyewe imekuwa kwenye kipaumbele kimojawapo. Kila mwananchi anahitaji kupata maji safi na salama. Tukiwa na maji safi na salama, tutapunguza magonjwa

ya mlipuko, tutakuwa na afya nzuri ambapo tutaweza kuendeleza maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kilimo, ni kweli tumeendelea kusema kilimo ni uti wa mgongo, tumesema kuwa kwa upande wa bajeti hii itashirikiana pamoja na mashirika yasiyo ya Kiserikali kusudi kuwekeza kwenye kilimo cha mpunga pamoja na miwa. Hapohapo tukifanya hivyo, tutakuwa tunapunguza mfumuko wa bei. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, sasa hivi kutokana na Tanzania kukumbwa na mambo ya tabia nchi ambayo yanatokea kwenye Mikoa na Wilaya mbalimbali hasa suala la ukame, kilimo cha umwagiliaji sasa ni muhimu sana. Inabidi kipewe kipaumbele kama bajeti inavyosema. Tukidumisha kilimo, ajira zitapatikana kwa vijana, ajira zitapatikana kwa wananchi wote kwa sababu kilimo ndio hasa wananchi wote hata ninyi mlio humu Bungeni Waheshimiwa Wabunge mko hapa kwa sababu ya kilimo. Kilimo ndicho kimewasomesha na ndio mko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuendelee kukipa kilimo kipaumbele. Zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wanaishi vijijini na wote wanategemea kilimo. Kwa hiyo, bajeti hii kadri inavyolenga kwenye mambo ya kilimo, mazao yanayoliwa kwenye mambo ya kilimo yatapewa thamani na tutaweza kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha taifa pamoja na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha misitu, naomba sana tukipatie kipaumbele kama bajeti inavyosema kwa

sababu misitu nayo inasaidia kupandisha kipato cha Tanzania na Mtanzania mwenyewe pamoja na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya viwanda na hasa viwanda vinavyotumia malighafi ya nchi yetu, tukiweza kuviwezesha hivi viwanda na kuvitengeneza na kuvifufua, tutaweza kuwapa wananchi ajira na hasa vijana ambao mpaka sasa hivi vijana wengi hawana ajira. Kwa hiyo, naishukuru Serikali yetu kwa kuweza kufikiria kuwa itaweza kuweka kipaumbele katika viwanda ambavyo vinatumia malighafi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii. Hasa tumesema pia tutaweza kuangalia mambo ya utafiti pamoja na huduma mbalimbali hasa kwenye mambo ya wataalam. Tukikazia hapohapo tutapata wataalam wengi na tumesema kuwa wataalam kwenye madini, wataalam kwenye *uranium* na wataalam kwenye gesi, kwa hiyo, mambo ya *training* yatakuwa hapohapo, tutaweza kupata wataalam wengi kutoka hapa nchini. Kwa hiyo, vijana wote walio huko nje, vijana wote wanaonisikia, kazi zitakuwepo kama tutaweza kukazania kwenye mambo haya ya rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni utalii. Utalii mara nyingi tulikuwa tunakazania utalii wa Kaskazini lakini bajeti hii imesema kuwa itadumisha na kuimarisha utalii, itaweza kuangalia vyanzo vingine vya utalii. Kusini kuna utalii, hata katikati ya nchi kuna utalii. Kuna utalii

wa Ruaha ambao mlikuwa mnauona kwenye luninga hivi karibuni. Kwa hiyo, hii bajeti mimi naiunga mkono na ninaona kuwa hii bajeti inawafaa Watanzania wote kila upande. Hii bajeti pia imeongelea kuhusu wafugaji, ingawaje wasemaji wengine wamesema haikuongelea ufugaji. Imeongelea na wavuvi, nikisema wafugaji namaanisha na wafugaji wa nyuki na wafugaji wa samaki. Kwa hiyo, hata wale wenye kipato cha chini wataweza kunufaika kutokana bajeti hii ila tunasema hivi wafuge kilimo cha tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamezingatiwa kwenye bajeti hii ambayo ni mazuri na yatawanufaisha wananchi. Kitu ambacho naomba, wananchi tufanye kazi, tupende kufanya kazi. Baada ya hapo, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa kaka yangu Dkt. William Mgimwa pamoja na Manaibu Waziri wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya, wametutayarishia bajeti ambayo haina shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo nilizozitoa, katika bajeti hii nimeona kuna baadhi ya maeneo ni changamoto. Eneo la kwanza, linahusu umeme. Pamoja na hela nyingi walizozitenga katika

eneo la umeme, lakini pale pana changamoto. Bado Serikali haijaonyesha dhamira ya kweli ya kutaka kutatua tatizo la umeme. Hakuna umeme rahisi katika dunia kama umeme wa makaa ya mawe. Umeme wa makaa ya mawe ni rahisi sana na kama Serikali ingeamua kwa dhati kutoa shilingi bilioni 70 ya kujenga *transmission line* ya kutoka Makambako mpaka Songea tungepata MW 120 ambazo zingeingia kwenye *grid* ya taifa. Nina hakika kabisa ingepunguza sehemu ya tatizo la umeme. Umeme huu ni rahisi kuliko umeme mwingine wowote. Tukifanikiwa kupunguza gharama za umeme *automatically cost of production* itakuwa imepungua na itasaidia viwanda vyetu kuzalisha bidhaa hapa nchini kwa bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni eneo la viwanda. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeendelea bila kufanya mapinduzi ya viwanda, lakini ni jambo ambalo katika nchi yetu halipo kabisa. Ukiangalia bajeti ya Viwanda ni ndogo sana. Kwenye viwanda ndiko utapata ajira, kwenye viwanda ndipo tunapata mapato lakini Serikali haijataka kuelekeza nguvu zake nyingi katika eneo hili. Naishauri Serikali iangalie upya kuwekeza katika eneo hili kwa sababu tutaongeza mapato na kwa wakati huohuo tutaongeza ajira kwa vijana wetu. *SIDO* imetapakaa nchi nzima lakini bajeti iliyowekwa kwenye *SIDO* inasikitishwa sana. Naiomba sana Serikali iangalie katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipo hapohapo kwenye eneo la viwanda, Serikali haijaonyesha dhamira ya kweli ya kutaka kulinda viwanda vyetu vya hapa nchini.

Tulikuwa na viwanda 21 vya *textile*, sasa hivi tumebakia na viwanda vitano (5). Viwanda vyetu, hakika vinashindwa kushindana na viwanda vya nje. Mimi na Kamati yangu tulipata nafasi ya kutembelea baadhi ya viwanda vya *textile*, tulisikia malalamiko yao kwamba nguo ambayo inatengenezwa hapa nchini inakuwa bei ya juu kulinganisha na nguo inayotengenezwa nje ya nchi. Serikali ilikuwa haina sababu ya kuweka *VAT* kwenye bidhaa ambazo zinazalishwa hapahapa nchini. Naishauri Serikali na naiomba ituondolee *VAT* kwenye bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Asilimia 30 ya pamba, ndiyo inatumika kwenye viwanda vyetu na asilimia 70 inauzwa. Sasa tukiweza kuongeza viwanda vingi vitakavyozalisha nguo hapa nchini, *automatically* tutakuwa tumeweza kuongeza viwanda vingi hapa nchini. Kwa hiyo, naishauri sana Serikali iondoe kabisa kodi ya *VAT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niko hapahapa kwenye viwanda, vilevile Serikali inatakiwa iangalie malighafi ambazo zinaagizwa nje ya nchi kwa ajili ya uzalishaji mali katika viwanda vyetu hapa nchini. Naishauri sana Serikali iangalie upya masuala ya ushuru.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezungumza vizuri sana kuhusu namna ambavyo imejielekeza katika kutatua tatizo la mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya shilingi. Ni kweli wameeleza vizuri, lakini jambo hili halitatekelezeka kama matumizi ya fedha za kigeni yatatawala katika nchi yetu. Ukienda nchi yoyote duniani, ukifika *airport*, hela mama ya ile nchi ndiyo inaanza kupata thamani, lakini hili jambo halipo katika nchi yetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imetawaliwa na utawala wa *dollarisation*, hata kupangisha nyumba zetu kwenye maeneo yetu unasikia mtu anataka *dollar* 200, 300. Kama hatutaliangalia jambo hili kwa upana wake, hakika hela yetu itaendelea kushuka thamani na haya tunayoyazungumza leo hii yatakuwa vichekesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni mgawanyo wa rasilimali. Bajeti hii ni kubwa, lakini inaonekana kwamba kuna baadhi ya maeneo yanapendelewa zaidi kuliko maeneo mengine. Hili jambo lina athari kubwa katika nchi yetu. Ukiangalia katika maeneo ya kwetu, kuna viwanda vikubwa kwa mfano *MPM* ambavyo vinachangia uchumi mkubwa katika nchi hii. Kuna viwanda vya chai, mbao, lakini hali ya barabara ni mbaya na tunashangaa kabisa kuona tunazalisha hela nyingi, tunaingiza hela nyingi kama walipa kodi lakini hela zinaenda kufanya kazi katika maeneo mengine. Tunaiomba sana Serikali iangalie jambo hili. Hata pale mjini kwetu Mafinga, ukienda utakuta barabara mbaya, kila tukiwaambia wenzetu hawataki kutusikia.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuamua kuchukua barabara ya eneo la Kinanyambo C mpaka Kisusa, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yameongelewa na wezangu, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, naiunga mkono bajeti. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, nampongeza kwa kuchaguliwa kwake na Manaibu wake kwa bajeti nzuri ambayo imelenga Watanzania wanyonge.

Mheshimiwa Spika, napenda niende moja kwa moja kwenye hoja. Jimbo la Morogoro Mjini lina wafanyabiashara ndogondogo. Katika bajeti hii nimeona wafanyabiashara ndogondogo kama bodaboda, naomba nao tuweze kuwanyanyua kwa kuwatolea kodi.

Mheshimiwa Spika, kwenye ajira za vijana, vijana wengi hawana kazi na njia ya kuweza kuwasadia ni kilimo na kuwapa mikopo ya kuweza kulima kwa kuwaunganisha kwa vikundi. Ardhi tunayo kubwa sana, tutaweza kunyanyua kipato na wakapata ajira. Uchumi wa kilimo ndiyo njia fupi ya kuweza kutoa ajira nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia wanawake nao wawezeshwe kupata mikopo na hususani katika Jimbo langu la Morogoro Mjini, wanawake wengi wanategemea biashara ndogondogo. Nao vilevile tuweze kuwapatia mikopo waweze kujiajiri. Tuongeze nguvu katika mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, tujitahidi sana kuziba mianya na hususani mapato ya Halmashauri ili tuweze kufikia malengo

ambayo tunayapanga ya kuwaokoa Watanzania katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwenye miundombinu, namuomba Mheshimiwa Waziri anikumbuke kwenye barabara zetu na hususani barabara ya Morogoro ambayo imechongwa, ni nyembamba mno. Ukipita mkokoteni, gari haipiti na barabara iko Mjini kabisa, nadhani Waheshimiwa wengi mmepita mmeiona.

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu pia namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie madawati ili Walimu na wanafunzi waweze kusoma vizuri katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya afya, tuna hospitali yetu ambayo ni ya Rufaa. Sasa hivi ina upungufu mwingi sana, katika bajeti hii, ningeomba nayo Mheshimiwa Waziri atufikirie maana anayewahi maji, anakunywa maji mazuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja asilimia 100 kwa 100. *(Makofi)*

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti hii iliyo mbele yetu. Naomba nichukue nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuleta bajeti nzuri, mimi naiunga mkono bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kinachoandaliwa na binaadamu, huwa hakikosi upungufu, lakini wamejitahidi, wameandaa bajeti nzuri. Naomba na mimi pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri

Mgimwa kwa kuchaguliwa kuwa Waziri na pia Manaibu wake nawapongeza kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza ni-*declare interest* yangu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Mimi natoka kwenye eneo ambalo tunalima pamba, pamba ni tatizo. Naomba nitangaze kwamba wananchi hawatauza pamba chini ya shilingi 1000/=. Tunaomba Serikali iingilie suala hili, iliangalie kwa karibu sana, ni tatizo, Wasukuma hatutauza pamba chini ya shilingi 1000/=. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze pia Serikali na nitambue kwamba hakuna maendeleo bila kukopa. Niseme hilo kwa sababu Serikali imepanga bajeti yake kwa kukopa pesa. Mimi naomba niseme, kwanza niipongeze Serikali kwamba ina sifa ya kukopesheka ulimwenguni, hiyo niipongeze Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu pesa nyingi zimemegwa kutoka kwenye miradi ya *ASDP, DASIP* kwenda kwenye mradi wa *SAGCOT.* Naomba Serikali mwaka kesho wasirudi tena kwenye bajeti hapa wakaja na *SAGCOT* tu, kwa sababu miradi mingi kwenye Wilaya zetu zimemegwa pesa zimeenda kwenye *SAGCOT*. Sasa tunaomba mwaka kesho wasirudi tena wakasema *SAGCOT* wanataka fedha zingine. Tunaomba mwaka huu waweze kuimarisha huo mradi wao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kwimba wameniomba mambo yafuatayo niyalete hapa,

niiiombe Serikali. La kwanza, wanaomba kodi ya bodaboda ifutwe, kodi ya bodaboda inasumbua, ni usumbufu. Wale wafanyabiashara wa bodaboda ni wajasiriamali, wanatafuta maisha kwa shida, naomba kodi yao ifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kodi ya mazao ni usumbufu mkubwa kwa wananchi. Mimi nashauri kodi ya mazao, fungu lililopangwa kwenye kodi ya mazao litafutwe sehemu nyingine kama ingewezakana kodi ya mazao pia ingefutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, uwanja wa ndege wa Mwanza. Miaka mingi imekuwa ni hadithi, tunaambiwa kwamba unajengwa, unajengwa, mwaka huu imepangiwa fedha, tunaomba mwaka huu hizo fedha zifike na uwanja wa ndege wa Mwanza uweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, reli pia imepangiwa bajeti kubwa mwaka huu karibu shilingi bilioni 130 na tumeahidiwa kwamba mpaka Disemba reli itafika Mwanza. Naomba Serikali ituahidi reli hiyo itafika Mwanza kwa sababu inapofika Mwanza inapita kwenye Wilaya yangu ya Kwimba, wananchi wangu watafaidika, watapata tija, naomba hilo pia lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme. Umeme Vijijini tumeahidiwa kwenye Wilaya yetu ya Kwimba hususani kwenye Tarafa ya Mwamashimba, kwenye Mji Mdogo wa Ngurumarwa, wameshafanya usanifu, wakasema mwaka huu wataleta umeme. Mwaka huu unakwisha

bado umeme haujafika. Naomba mwaka ujao, bajeti ya 2013/2014, naomba mradi wa umeme Ngurumarwa ukamilike. Pia tuna jenereta mbili ziko kwenye Tarafa ya Mwamashimba, nao wamefanyiwa usanifu ili waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusu masuala ya makampuni yanayotoa huduma ya simu. Haya makampuni yanayotoa huduma ya simu yanafanya biashara ya *M-PESA*. Biashara ya *M-PESA* wanafanya kazi na kwa siku wanapata karibu shilingi bilioni nne (4). Naomba Serikali iweze kunifafanulia kwamba hiyo huduma wanayotoa, wanapewa masharti yanayofanana na mabenki kwa sababu wanafanya shughuli inayofanana na mabenki? Je, kama wanalipa kodi, wanasimamiwa na Benki Kuu kuhakikisha kwamba hizo pesa za wananchi ambazo ziko kwenye miradi hiyo hazipotei? Kwa sababu juzi kampuni mmoja ya simu imefanya biashara ya shilingi trilioni 6.6 sasa ningependa kujua Serikali imetoza kodi shilingi ngapi pale na pia hiyo huduma inasimamiwa vipi kwa sababu hiyo huduma inaweza hata pia ikapitisha pesa chafu ikahatarisha usalama wa nchi. Kwa hiyo, ni muhimu kujua ile pesa inasimamiwa vipi kuhakikisha kwamba inatumika inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, sina mengine ya kusema, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo!

**SPIKA**: Mheshimiwa Hamad!

**WABUNGE FULANI:** Sio Hamad.

**SPIKA:** Nani?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Ndassa!

**SPIKA:** Basi nimekosea.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA**: Mheshimiwa ulishaongea, siwezi kukupa nafasi.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo.

**SPIKA**: Mwongozo wa nini tena? Haya!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu tangu Jumatatu tulipoanza kuzungumzia bajeti, Waheshimiwa Wabunge wengi hasa wanaotoka Kanda ya Ziwa, wamezungumzia sana kuhusu suala la zao la pamba kuhusu msimu kuanza na kwa sababu kama nilivyosema zao hili linalimwa karibu Wilaya 42, linawahusisha Watanzania milioni 16 na pamba yao kwa hivi sasa bado iko majumbani. Nini kauli ya Serikali

kuhusu bei ya pamba lakini lini msimu uanze? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Mbunge, mimi natoaje mwongozo kuhusu kauli ya Serikali? *(Kicheko)*

Hapana, mimi sina mamlaka kuhusu kauli ya Serikali, nadhani watatumia utaratibu unaohusika.

Haya nimwite sasa Mheshimiwa Hamad Ali Hamad.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia jioni hii au mchana huu nami kupata nafasi ya kusema machache kama mchango wangu ndani ya bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwenda kwenye bajeti, naomba niwaombe Wabunge wenzangu kwamba tunapokuwa tukichangia iwe bajeti au mijadala mingine, tuzingatie zaidi maslahi ya umma wa Watazania kuliko kujiangalia sisi wenyewe na maslahi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana wakati Mheshimiwa Mbunge mwenzangu mmoja akichangia bajeti hii, kama vile haelewi taarifa za maeneo mbalimbali ya Watanzania, alisema wazi kwamba hakuna Watanzania wanaokufa kwa njaa katika Tanzania hii lakini leo asubuhi Mheshimiwa Mbunge mmoja vilevile alipokuwa akiuliza swali kwa Waziri Mkuu, alisema wazi kwamba kuna matatizo katika maeneo yake na watu wanakufa kwa njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakuwa hatueleweki. Wananchi watakuwa hawatufahamu vizuri. Jambo hili lilionesha kwamba kulikuwa na hoja ya maslahi binafsi kwa sababu Mbunge aliyesema kwamba hakuna anayekufa kwa njaa alisha-*declare interest* yake kwamba yeye ni mfanyabiashara. Mfanyabiashara wa namna hiyo, anaweza akasababisha wananchi kushindwa kununua bidhaa kwa sababu ya kutokujali maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nami niende kwenye hotuba hii ya bajeti. Kila Mbunge hapa, kila siku tunaopata muda wa kuuliza maswali iwe ya kawaida au ya nyongeza, lakini hata tunapokuwa tukichangia hoja mbalimbali, tunakuwa tukionesha matatizo mbalimbali katika maeneo yetu na tunakuwa tukiiomba Serikali kwamba, ifanye jitihada za makusudi ili kutatua matatizo hayo. Hii ni kuonesha kwamba, fungu la maendeleo la bajeti, halikidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau. Naomba niseme kwamba, siiungi mkono bajeti hii kwa sababu Watanzania huko nje ambao wana matatizo mbalimbali hawana matumaini ya kutatuliwa kero zao au mahitaji yao kwa bajeti hii na fungu hili la maendeleo. Fedha ya maendeleo au fungu la maendeleo, ndilo ambalo tunatarajia lijenge barabara zetu, lijenge reli, lijenge shule na zahanati, lisambaze maji safi na salama mijini na vijijini na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kila mwaka inatumia fedha nyingi kwa kukarabati barabara. Hii si kwa sababu ya ujenzi wa chini ya kiwango tu cha barabara zetu, lakini barabara zinaelemewa na mzigo mzito wa kulazimisha kupitisha *cargo* kwa magari au malori. Mizigo ambayo ingestahili isafiri kwa treni au kwa njia ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiiangalia barabara ya kutoka Dar-es-Salaam kuja Dodoma, ina matuta, imechanikachanika na inaonekana wazi kwamba, usipokuwa dereva mwangalifu, unaweza ukapata ajali kwa barabara hii. Mimi siamini kwamba ni kwa sababu ya ujenzi wa chini ya kiwango wa barabara hizi lakini naamini ni kutokana na mizigo mizito inayopita kwenye barabara hizi saa 24. Lakini tutawezaje kuwa na mbadala wa kupitisha mizigo kwenye barabara hizi kama hatukuwa madhubuti na makini, tukaweza kujenga reli zetu? Pia hatuwezi kujenga reli kama hatukuwa na fungu kubwa la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote hapa huwa wanawasilisha matatizo na kero zilizopo katika maeneo yao, wakionesha kwamba, wakulima wanapata shida ya kuyafikia masoko kwa sababu ya kukosa barabara, kwa sababu ya kukosa reli. Kwa sababu hizo, wakulima wana-*mark time* na hawafikii kwenye maendeleo wanayoyatarajia kwa jasho lao au kwa bidhaa wanazolima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Suala la nidhamu ya matumizi ni jambo ambalo

linapoteza pesa nyingi za umma na fedha hazifiki kwenye maeneo tarajiwa kwa sababu, wenzetu ambao tumewaamini na kuwapa mamlaka ya kusimamia fedha hizi, wanakuwa kama vile panya, wanakula fedha hizi kinyume cha utaratibu, wanawaacha Watanzania na matatizo yasiyokwisha. Kama hatukuwa madhubuti na kwa mtindo wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, wa kuoneana aibu kwa watendaji, kila siku tutakuwa tukionesha matatizo yasiyokwisha kwa sababu ya kukosekana kwa uzalendo wa dhati wa watendaji ambao tunawapa mamlaka hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wapya waliochaguliwa juzi na Mheshimiwa Rais, naomba niwaambie kuchaguliwa kwenu ni changamoto kubwa. Mawaziri ambao wamefanyiwa mabadiliko, haikutokea tu kama ndoto kutoka kwenye usingizi wa Rais lakini ilitokana na namna Wabunge tulivyoonesha kwamba, hawakuwa waadilifu na hawakuwa wazalendo wa kweli, katika kuhifadhi fedha za umma katika Wizara walizokuwa wakizisimamia. Naomba niseme Mawaziri wapya, Watanzania wanatarajia kwamba, mtakuwa waadilifu na waumini wa kweli wa fedha za umma katika kuzilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna ambavyo tunakuwa tukikusanya fedha, naomba nisema kwamba, Mamlaka na Taasisi tulizozipa mamlaka ya kukusanya fedha, zinainyima Serikali mapato makubwa. Ni kwa sababu wametengeneza mitandao yao ya urasimu katika kukusanya kodi. Urasimu katika kukusanya kodi unawafanya wafanyabiashara watafute njia mbadala

ya kuendesha biashara zao. Njia hizi mbadala ndizo njia ambazo zinainyima mapato Serikali na kusababisha fedha nyingi kuvuja na kuingia kwenye mifuko ya wajanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Eeeh, Taarifa! Muda wenyewe hautoshi, Mheshimiwa!

**MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge lako hili Tukufu liko kwa ajili ya kujadili Watanzania walio nje ya Bunge hili, takribani milioni 45 na miongoni mwa Watanzania hao milioni 16 ni Watanzania wanaolima pamba na hivi sasa wana dharura kubwa ya kutouza pamba yao ili wakidhi mahitaji yao baada ya kuhangaika kwa muda mrefu kuilima pamba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu sasa, naomba Bunge lako hili Tukufu, kwa sababu liko kwa ajili ya Watanzania wengi, Bunge hili liweze kujadili suala hili ili hawa Watanzania milioni 16 wa pamba waweze kunufaika na pamba yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa! Matumizi mabaya ya Taarifa kwa sababu mimi nilifikiri unampa Taarifa huyu

aliyemaliza kusema, kumbe sio. Ni matumizi mabaya. Mheshimiwa Kabaka!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo. Mimi nitajikita hasa kwenye kipengele kimoja ambacho kimezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini pia katika maoni ya Kambi ya Upinzani suala hili limejitokeza. Pamoja na kwamba, muda wa Wizara yangu bado lakini nimeona nilitolee ufafanuzi hapa kwa sababu limejitoikeza katika bajeti hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi nalo ni kuhusiana na suala zima la pensheni ya wazee.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM, ukurasa wa 98, Kipengele C, Chama kimeelekeza Serikali kupitia Wizara yangu ya Kazi na Ajira, ipanue wigo wa hifadhi ya jamii kwa wananchi wake. Muswada uliohusu Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao ulipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, ulikuwa na lengo hilohilo.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la pensheni ya wazee ambalo limezungumziwa katika majadiliano haya, kwa kweli ni jambo nyeti na ninakiri kwamba linahusu pia Hifadhi ya Jamii. Hata hivyo, ninaomba niongezee kwa kusema kuwa, suala hili haliwezi kufanyika kwa kukurupuka, ni lazima kuliandalia utaratibu ambao utasaidia kulifanya suala lenyewe liwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika maoni ya wenzetu Kambi ya Upinzani ambapo wameweka

ukurasa wa 32, Kipengele cha 5, wamesema tu kwamba bajeti hii pia ingetoa pensheni kwa wazee lakini wenzetu hawakutueleza *definition* ya hawa wazee ni akina nani? Ni wangapi? Umri gani na kiasi gani cha fedha, ingawa kuna Msemaji mmoja amezungumzia shilingi bilioni mbili. Kuna tafiti zimeshafanyika, kuna wengine wanasema tuna wazee 2,000,000, kuna wengine wanasema 2,400,000, sasa ukiiangalia hiyo shilingi bilioni mbili iliyozungumziwa, ukiwagawia wazee 2,000,000 na ninafikiri walimaanisha mwezi mmoja, kila mzee atapata shilingi 1,000/= na sidhani kama sisi Watanzania tunataka wazee tuwape shilingi 1,000/= kila mwezi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa kwa kufikiria hili na hasa baada ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, suala zima la pensheni zote, ikiwemo hii ya wazee, limechukuliwa na Mamlaka hii na kazi ambayo inafanyika ni kupitia tafiti zilizokwishafanywa. Tafiti zimefanyika, Serikali imefanya, lakini pia imesaidiana na *Heritage International* pamoja na wadau wengine na kazi ya *SSRA,* Mamlaka hii, ni kupitia tafiti hizi. Ili sasa kujaribu kuangalia maoni yaliyotolewa, lakini na wao wenyewe kama wataalam waweze kufanya tafiti zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki tunachoongea *SSRA* wameshapita Kanda tatu kati ya Kanda saba. Katika mapitio yao wanakopita, wanakutana na Mabaraza ya Wazee, wanakutana na Halmashauri ambazo ndio zinawahodhi hawa wazee na wanajaribu kuangalia mambo kadhaa muhimu ambayo ni

muhimu kabisa kabla hujaanza kutoa pensheni ya wazee.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mambo hayo...

**TAARIFA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja amalize kusema kwa sababu muda wenyewe ni mdogo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Naomba amalize, halafu Taarifa utatoa baadaye.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mojawapo ya mambo muhimu ambayo Mamlaka inajielimisha nayo, ni namna ya kuwatambua wazee, yaani *identification,* ikiwemo umri, idadi yao, mahali walipo na hii itasaidia tuanze na wazee wa umri gani. Pili, ni kuangalia miundombinu iliyopo katika Halmashauri zetu, Kata, Vitongoji, ambavyo vitasaidia usimamiaji wa utekelezaji wa pensheni hii ya Wazee. Tatu, ni namna ya kupata na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali na hapa *ICT* ni lazima itatumika kama *infrastructure.* Nne, kuna kitu ambacho kinaitwa *cash transfer* ambacho kinafanyika sasa hivi kwa majirani zetu Kenya. Wanapeleka pesa taslimu moja kwa moja kwa wazee wahusika na kwa nchi ya Kenya, wamechukua wale wazee tu ambao hawajiwezi. Kwa

hiyo, na sisi tunajaribu kuona je, tufanye hii *cash transfer?* Kama tutaifanya, *mechanism* yake itakuwaje? Kwa hiyo, hapa tunaangalia ni miundombinu ipi itakayotumika, ili tutumie kuwapa hawa wazee. Kama ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii au kama ni kupitia katika *SACCOS* na mambo kama hayo. Tano, ni lazima tujielimishe kuhusu gharama ya pensheni. Hii inajumuisha gharama ya pensheni yenyewe halisi, lakini pia na *administrative cost* kwa sababu, unapopeleka hela lazima kuna gharama za kupeleka hiyo hela; isije ikawa unapeleka shilingi moja, unatumia shilingi moja hiyohiyo, haitaleta tija. Pia ni lazima tujielimishe kuhusu vyanzo vya hii pesa, tutaitoa wapi? Wenzetu Kenya, wametumia wafadhili ndio wanawapa pesa kwa ajili ya hii *cash transfer.* Je na sisi tungependa tutumie wafadhili? Ni *sustainable* kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa hivi hadi tunapoongea, tumefikia hatua nzuri na kutokana na ufinyu wa bajeti, mwaka huu hatukuweza kufanya kazi hiyo, lakini ninasema pia hatukuwa na maandalizi ya kutosha. Lakini imebidi kufanya kazi kikanda, kama nilivyosema na tumeshapitia Mikoa mingi ikiwemo Rukwa, Mtwara, Dodoma, Manyara, Kagera, Pwani na Dar-es-Salaam. Tumeshatuma dodoso au *questionaire* katika Wilaya zote za Mikoa hii ili kukusanya taarifa hizi nilizozitaja hapa.

Mheshimiwa Spika, timu ya *SSRA* pamoja na Wizara ya Kazi, kwa sasa wapo Mkoa wa Pwani na Dar-es-Salaam na tunatarajia mara tutakapopata tozo baada ya Sheria hii kusainiwa, maana hatujaarifiwa

kama ule Muswada umeshawekwa saini na Mheshimiwa Rais, ili kuruhusu tozo. Kwa hiyo, mara tutakapopata tozo sasa tutajua kwamba, tuna pesa, *SSRA* watakuwa na pesa na kazi hii itafanyika kwa haraka na wepesi zaidi. Hatua zinazofuata baada ya hili, baada ya kupata taarifa kutoka *SSRA,* baada ya kukusanya taarifa hizi, sasa tutaanza kuwapata wadau watakaosimamia kwanza ulipaji, lakini wadau watakaotoa pesa na wadau watakaopima matokeo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hatua zote hizi zitahakikisha wazee wanawakilishwa ipasavyo na baada ya hapo kama mnavyojua, hii ni shughuli ambayo inahusisha nchi nzima, bajeti ya Hazina, kwa hiyo, ni lazima tuandae Waraka wa Baraza la Mawaziri. Hatua za Waraka tunazifahamu ambazo zitasaidia sasa kuandaa bajeti na gharama nzima ya pensheni pamoja na miundombinu pamoja na masuala ya utawala. Lazima tuwe na *a focal person* katika kila eneo ambaye atatusaidia kuwafikia wale wazee. Hii ni sehemu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba kama fedha zitapatikana kama ilivyopangwa, tutaweza kuleta mrejesho Bungeni juu ya namna ya utekelezaji wa pensheni hii utakavyofanyika katika Bunge la Juni, 2013. Tukumbuke kwamba, kazi hii sio nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kinachogawiwa hapa ni *adendum* ya hotuba ama mawasilisho ya hotuba ya Kambi ya Upinzani. Nilikuwa nimeeleza wakati ule kwamba, taarifa zote zinazokuwa *laid on the Table,* kama kwa sababu moja au nyingine kumetokea makosa katika zile taarifa, utaratibu wetu tunaweka *adendum,* ndio hii inayogawiwa sasa.

Mheshimiwa Zitto, dakika moja, maana muda umeisha. Taarifa yako inasemaje?

**TAARIFA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kazi, ameitoa. Nampongeza kwa kupokea mapendekezo ya Kambi ya Upinzani ambayo tumeyatoa toka mwaka jana kuhusiana na pensheni kwa wazee. Pia nampongeza kwa kumkosoa Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi ambaye aliponda sana wazo hili juzi kwa kuonesha kwamba haiwezekani kuwa na pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, ila nilikuwa naomba tu kumpa taarifa kwamba hakuna Mbunge yeyote wa Kambi ya Upinzani ambaye alisema kwamba pensheni hiyo itakuwa ni shilingi bilioni mbili. Pendekezo la Pensheni kwa wazee sio jipya, ni pendekezo ambalo tulilitoa mwaka jana na tulielezea idadi ya wazee ambayo ipo nchini na tulielezea gharama ambazo zitatumika kwa ajili ya pensheni hiyo na tulielezea vyanzo gani vya mapato, tulitoa, marehemu Regia Mtema, alipokuwa Waziri Kivuli wa Kazi, aliainisha vyanzo vitatu vya

mapato ambavyo vinaonesha ni wapi ambako tutapata fedha kwa ajili ya pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, si kweli kwamba tunataka wazee wapewe shilingi 1,000/= kama Mheshimiwa Waziri anavyosema na ninamheshimu sana mama yangu huyu, sitarajii kama anaweza kwa makusudi kabisa akapotosha mambo ambayo tumeyasema. Tulisema chanzo cha kuanzia pensheni kwa wazee kiwe ni angalau shilingi 20,000/= kwa idadi ya wazee ambao wanaanzia umri wa miaka 60 na kuendelea au miaka 65 na kuendelea lakini nashukuru kwamba wamelitambua jambo hili na wamelipokea na ni vizuri kwa Serikali iliyoko madarakani kupokea mawazo ambayo yanatoka Kambi ya Upinzani, kwa sababu tunajenga nyumba moja, nchi yetu ni yetu sote, sisi sote ni Watanzania na lengo letu ni kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimikwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kweli haikuwa taarifa, ilikuwa hotuba ndogo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, jana Naibu Spika alipokaa hapa tulifunga kupokea maombi ya kujadili na sababu zenyewe ni kwamba tulikuwa tunarudia tu, tunarudia tu! Halafu tukazingatia kwamba hawa tuliokuwa tunawasemea maneno yetu haya yote kuanzia Waziri, mgeni, Manaibu wake, wageni, ili angalau bajeti ipate uzito unaostahili. Kwa hiyo, tunaahirisha kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi ili

kusudi hawa wenzetu waanze kujiandaa na kesho nitakuwa na watu wengine ambao watakuwa upande wa Serikali wanajibu baadhi ya hoja mlizokuwa mmetoa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 22Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*